




## Alichokisema Waziri Mabula hati za viwanja

UKURASA 3



Jumapili Septemba 4, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581058

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

## Harmonize aitwa kuimba Injili

UKURASA 20



# Askofu aanguka kanisani, afariki

• **Ni** wakati wa ibada ya mazishi ya kiongozi wa... *Endelea uk. 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### AJALI YA BASI, FUSO ILIVYOUA WATU WATANO, KUJERUHI 54

WATU watano wamepoteza maisha huku 54 wakijeruhiwa katika ajali iliyohusisha basi na lori aina ya fuso yaliyogongana uso kwa uso eneo laIbadakuli, Manispaa ya Shinyanga...

UKURASA WA 8

### MTUMISHI ADAIWA KUNASWA RUSHWA

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, amesema ndani ya saa tatu wamemkamata mtumishi wa serikali akiwa amejiingizia rushwa ya Sh. 960,000 na orodha ya wengine 14 inatarajiwa kuanikwa kesho...

## Mzee wa Upako atia mkono tozo

UKURASA 3




Basi la Super Najimunisa (kulia) likitokea Dar es Salaam kwenda Mwanza, likiwa limegongana uso kwa uso na Fuso katika eneo la Ibadakuli, Manispaa ya Shinyanga jana majira ya saa 8:00 usiku likitokea Mwanza kwenda Dar es Salaam likiwa limebeba shehena ya dagaa na kusababisha vifo vya watu watano na majeruhi 54. **PICHA : MARCO MADUHU**



## Rais Samia aagiza tathmini UVIKO-19

UKURASA 2

**MICHEZO** TAIFA STARS 'OUT' MICHUANO CHAN UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akipata maelezo kuhusu matumizi ya vifaa mbalimbali vya Uvuvi kutoka kwa Mkuu wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar KMKM wakati alipotembelea mabanda ya maonesho kwenye Tamasha la Siku ya Kizimkazi jana.
**PCHA: IKULU**

# Askofu aanguka kanisani, afariki dunia

**Na Waandishi Wetu**

SIMANZI na vilio jana vilitawala wilayani hapa baada ya Askofu wa Kanisa la Anglikana Tanzania (ACT) Dayosisi ya Mpwapwa mkoani Dodoma, George Chiteto kufariki dunia ghafla baada ya kuanguka kanisani.

Chiteto (59) ambaye Jumapili iliyopita aliwekwa wakfu kuwa Askofu wa Tatu wa Dayosisi ya Mpwapwa, alipatwa na mauti jana baada ya kumaliza mahubiri ya mazishi katika ibada ya mazishi ya aliyekuwa Rais wa Ushirika wa mama wa Kikristo wa kanisa la Anglikana Tanzania (UMASKI), Hilda Lugendo.

Mazishi ya Hilda, ambaye ni mke wa Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Southern Highliands, Mbeya, yaliongozwa na Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana Tanzania, Dk. Mahimbo Mndolwa, na baadaye alizikwa kijiji cha Mbwego wilayani Muheza.

Katika ibada hiyo, Askofu Chiteto alitoa mahubiri katika Kanisa la Kristo Mfalme, Mtaa wa Madaba. Wakati wa kumaliza mahubiri, alisema anatamani kufa kama alivyokufa Hilda ndipo alipokwenda kukaa katika kiti chake madhabahuni na kuzidiwa ghafla, kupoteza fahamu na kuanguka.

Baada ya kuanguka, alibebwa na wachungaji na maaskofu waliokuwa katika ibada hiyo na kumwingiza katika gari kisha kumpeleka Hospitali Teule ya Wilaya ya Muheza kwa matibabu.

Pamoja na kupelekwa hospitalini, shughuli zingine za ibada ikiwa ni pamoja na kutoa heshima za mwisho kwa mwili wa Hilda ziliendelea kanisani hapo zikiongozwa na zaidi ya maaskofu 20 wa kanisa la Anglikana kutoka dayosisi mbalimbali nchini.

Wakati shughuli hizo zikiendelea, Askofu Mkuu Dk. Mndolwa alisimama ghafla na kutangaza kuwa Askofu Chiteto amefariki dunia akiwa anapata matibabu hospitalini.

Hatua hiyo ilisababisha kanisa kukumbwa na vilio na majonzi kutokana kuwa muda si mrefu alikuwa madhabahuni pamoja na maaskofu wengine kwenye ibada ya mazishi ya kiongozi wa kanisa hilo.

Askofu Chiteto ameacha mke na watoto sita. Kabla ya kuchaguliwa kuwa Askofu Juni 26, mwaka huu, alikuwa Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana (SJUIT), Dodoma kinachomilikiwa na Kanisa la Anglikana Tanzania. Alikuwa na Shahada ya Uzamili katika Theolojia (Masters of Arts in Theology) aliyoipata mwaka 2012 katika chuo hicho.

**MAZIKO YA HILDA**

Akizungumza katika maziko ya Hilda Askofu Mkuu Dk. Mndolwa alisema kanisa limempoteza mtu muhimu lakini hakuna cha kufanya kwa sababu Mungu amempenda zaidi.

Dk. Mndolwa alisema Hilda ambaye alifariki dunia nchini Norway, atakumbukwa kwa mema aliyoyatenda enzi ya uhai wake. Aliwakumbusha Wakristo kuendelea kumcha Mungu ili kujiwekea njia ya kupata pepo kwa kuwa siku moja wataonja mauti.

Naye Askofu Lugendo ambaye ni mume wa Hilda, alisema amempoteza mke ambaye alisema waliishi vizuri katika maisha yao ya kumpendeza Mungu. Hilda ambaye alizaliwa mwaka 1965, na mume wake katika maisha yao ya ndoa walibarikiwa kupata watoto wanne.

Katika ibada na mazishi hayo, zaidi ya maaskofu 20 kutoka madhehebu mbalimbali, wakiwamo wa kanisa la Anglikana, walihudhuria kutoa ujumbe mbalimbali wa neno la Mungu.

Serikali iliwakilishwa katika mazishi hayo na Mbunge mstaafu wa Muheza na Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Umma, Balozi Adadi Rajabu, ambaye alitoa salamu kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwapa pole ndugu, familia na kanisa kwa msiba huo.

Kamishna huyo aliwataka familia hiyo kuwa watulivu katika kipindi hiki kigumu cha msiba na kwamba serikali inatoa pole kwa ndugu na familia.

**KILIO MPWAPWA**

Waumini wa Kanisa Anglikana Tanzania Dayosisi ya Mpwapwa, jana walijawa na simanzi baada ya taarifa za kifo cha Askofu Chiteto, aliyehudumu katika kiti hicho kwa takribani siku sita tangu ibada ya kuwekwa wakfu.

Taarifa iliyotolewa jana na Ofisa Habari wa Kanisa hilo, Michael Luoga, ilisema kuwa Askofu Mkuu Dk. Maimbo Mndolwa, anawatangazia waumini wa kanisa hilo nchini kifo cha Askofu Chiteto kilichotokea jana katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Muheza, Tanga.

Taarifa hiyo ilisema Askofu Mkuu Mndolwa alitoa taarifa ya kifo cha Askofu Chiteto kwenye misa ya kuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa UMAKI, Hilda Lugendo, iliyofanyika kwenye Kanisa Anglikana la Kristo Mfalme, Muheza, Dayosisi ya Tanga.

"Kabla ya kufariki dunia, Askofu Chiteto alishiriki misa ya kuaga mwili wa Mama Hilda Lugendo na kuhubiri katika misa hiyo kisha muda mfupi baada ya kumaliza hotuba yake, alikutwa na hali ya kupoteza fahamu kisha kukimbizwa hospitalini hapo. Muda mfupi baadaye, alifariki dunia," ilisema sehemu ya taarifa hiyo

Kutokana na msiba huo, baadhi ya Maaskofu wa Kanisa Anglikana Tanzania wamekutana na kufanya kikao cha dharula katika Kanisa Anglikana la Kristo Mfalme, Madaba Muheza, kupanga ratiba kamili ya mazishi kisha kuwajulisha rasmi waumini nchini kote.

■ **Imeandikwa na Stephen William, MUHEZA na Paul Mabeja, DODOMA.**

# Rais Samia aagiza tathmini UVIKO-19

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameiagiza Wizara ya Afya iangalie na itathmini hali ya UVIKO-19 ilivyo kwa sasa na kueleza kama kuna haja wananchi kuendelea kutumia barakoa au la.

Aliagiza hayo jana Wilaya ya Makunduchi, Mkoa wa Kusini Unguja, Zanzibar wakati wa kilele cha maadhimisho ya Tamasha la Kizimkazi yaliyobebwa na kaulimbiu 'Royal Tour na Uchumi wa Buluu ni Chachu ya Maendeleo'.

Katika maadhimisho hayo, Rais Samia aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya UVIKO-19 kwa kuwa tatizo hilo bado lipo.

"Nilipoingia eneo hili leo (jana), nilikuja na barakoa yangu, nikatazama uwanja, sikuona hata mmoja amevaa barakoa, isipokuwa mimi na timu yangu niliyokuja nayo.

"Kwa hiyo, mimi nikaanza kutoa yangu, wanasema 'ukienda kwa Waroma, fanya kama Waroma wanavyofanya', nikaanza kutoa ya kwangu na wengine wakanifuata.

"Hii inaonyesha nini? Ninataka niwaambie tusijiachie sana, bado janga lipo, tumejifunza kuishi nalo, lakini bado janga lipo. Niwaombe Wizara ya Afya waangalie mwenendo huu tunaokwenda nao, kuacha barakoa watu wote hawa, inaonyesha watu wamechoka nazo," aliagiza.

Rais Samia aliitaka wizara hiyo iangalie na itathmini hali ilivyo na waendelee kuwa nazo au kwa muda wananchi wapumzike.

"Ninalotaka kuwaambia, janga bado lipo, chanjo bado zipo, kama hujachanja kimbilia sehemu ya kuchanja, nenda kachanje, ni bure, hulipi hata shilingi, nenda kachanje janga bado lipo," alisisitiza.

**MAFANIKIO SENSA**

Mkuu wa Nchi pia aliwashukuru Watanzania kwa kutoa ushirikiano kwa makarani wa Sensa ya Watu na Makazi walipofika kwenye nyumba zao wakati wa kazi hiyo iliyoanza Agosti 23 mwaka huu.

"Wamepata ushirikiano mkubwa, wananchi walikuwa na hamasa kubwa na mchakato wa kuhesabu watu umekwenda vyema, ninatambua tumeongeza siku saba za kuchukua sensa za nyumba na makazi na hii ni fursa kwa wale ambao hawajahesabiwa, wahesabiwe tuweze kufanikisha kwa ufanisi," alisema.

Kuhusu tamasha hilo, Rais Samia alisema lina lengo la kuwaleta pamoja na kuwaunganisha wana Kizimkazi na maeneo ya jirani, wana Kusini na Watanzania kwa ujumla.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema wamempata Rais kutoka Kizimkazi ambaye ni mchapakazi na hodari na ameendelea kusimamia taifa kwa weledi mkubwa.

Alisema wananchi wa Kizimkazi wameonyesha mshikamano mkubwa kwenye tamasha hilo, pia akiahidi wataendelea kumsaidia Rais Samia usiku na mchana katika kuwatumikia Watanzania.

## HABARI KITAIFA

# Alichosema Mabula hati viwanja 20 kwa 20

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, amesema uwiano wa moja kwa moja wa kiwanja cha 20/20 haukubaliki, kwa sababu hakuna viwanja vyenye upana na urefu wa namna hiyo.

Kutokana na hali hiyo, ameagiza kampuni binafsi za upangaji, upimaji na zingine zinazojihusisha na masuala ya ardhi na yeyote anayejihusisha na uuzaji wa vipande vya ardhi kwa mtindo huo, kusitisha kazi hizo haraka na kurejesha fedha kwa wananchi kwa maeneo ambayo tayari kuna migogoro.

Waziri Mabula aliyasema hayo wiki hii mkoani Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa siku mbili wa wadau wa uendelezaji milki.

Alisema kwa mujibu wa sheria ya Mipangomiji Na. 8 ya mwaka 2007, Sura 355, kifungu Na. 77 (1) (b), (i), kanuni ya viwango vya upimaji maeneo, zilizotangazwa kwenye gazeti la serikali namba 91 na 93, Machi 9, 2018, ukubwa wa maeneo kwa matumizi mbalimbali umeainishwa.

"Kwa mujibu wa sheria hii na taaluma ya mipangomiji, viwanja vya matumizi mbalimbali vinatakiwa kuwa na ujazo tofauti, Ujazo wa Juu, Ujazo wa Kati na Ujazo wa Chini.

"Viwanja hivi vinatakiwa kuwa na mapana na marefu yenye uwiano wa moja kwa mbili mpaka moja na mbili na nusu.

"Kwa mfano, kiwanja chenye ukubwa wa mita za mraba 400 kinapaswa kuwa katika uwiano wa upana wa mita 16 na urefu 25, uwiano wa moja kwa moja 20/20 haukubaliki kitaaluma, hakuna kiwanja chenye upana na urefu ulio sawa," alisema na kuongeza kwamba taaluma ya mipango miji inaelekeza mpangilio wa viwanja kuhusiana na ujazo.

Waziri Mabula aliagiza bodi zote za kitaalam kuanzia Bodi ya Usajili Wataalam wa Mipango Miji, Baraza la Wapima wa Ardhi Tanzania na Bodi ya Usajili ya Wathamini, kufanya uchunguzi wa kampuni zote zinazofanya kazi kinyume na sheria ili hatua kali zichukuliwe haraka.

"Nitoe rai kwa wananchi, kuwa makini na watu wanaowauzia ardhi kwa aina hii, kabla ya kununua ardhi mwananchi hakikisha unapata taarifa au mwongozo kutoka ofisi ya ardhi ziliko Halmashauri au ardhi Mkoa ili kupata ushauri," ameshauri.

Kiongozi huyo alisema hivi karibuni kutokana na thamani ya ardhi kupanda kumekuwapo na idadi kubwa ya makazi ni uwapo wa kampuni binafsi za upangaji na upimaji ardhi.

"Kumetokea wimbi kubwa la uuzaji holela wa viwanja ambavyo havizingatii matakwa ya sheria ya mipango miji, kwa baadhi ya kampuni na wakala wa ardhi wamekuwa wakigawa na kuuza viwanja ambavyo havijapangwa wala kupimwa kwa jina maarufu 20/20.

"Hili ninalizungumzia kwa sababu viwanja ni fursa ya kujitafutia kipato, katika suala la kupanga viwanja 20/20, na wanakwenda maeneo ambayo pengine Halmashauri haijapima, wanawakatia watu na kuwauzia," alisema.

Alisema wanahitaji watu wapate viwanja ambavyo wanaweza kuzalisha shughuli za kiuchumi na si vya tamaa za fedha za haraka haraka.

"Kama wizara tumepiga marufuku, sitaki kuona wala kusikia, mpima yeyote atakayepitisha kiwanja cha aina hii 300, 400, 500, yaani katika upimaji wako huna ujazo wa juu, ujazo wa kati na ujazo wa chini kwenye maeneo yako?" aliwahoji.

Waziri Mabula alisema hivi karibuni wizara imekuwa ikipokea maombi kutoka kwa wananchi wakitaka kupimiwa maeneo yao, ambayo wanadai wameshauziwa lakini eneo halijapangwa wala kupimwa. Alibainisha kuwa kampuni hizo zimekuwa zikinunua maeneo na kukata viwanja vidogo vidogo vyenye ukubwa wa mita za mraba 300 bila kuzingatia sheria na mahitaji ya huduma za jamii kisha kuwauzia wananchi.

"Ukiangalia hakuna maeneo ya barabara na yaliyotengwa hayafiki hata mita nne kwenye eneo hilo, baada ya kuwauzia wananchi wanawaelekeza waende kwenye wizara kwa ajili ya kupimiwa. Wakati huo huo wameshauza na kuleta migogoro.

"Kampuni hizi tumeshazibaini na tutaangalia namna ya kuzichukulia hatua, nielekeze bodi zinazohusika kuanza kuwabaini mmoja baada ya mwingine kwa sababu wengine tunao kwenye mitandao, hili ni jambo ambalo haliakisi taaluma yako."

Waziri huyo alisema kampuni inapima ili ijipatie faida lakini anayepimiwa anaingia kwenye matatizo na mengine yanapimwa yakiwa na milki tayari.

Alimtaka Mkurugenzi wa Sekta Milki kwa kushirikiana na bodi zinazohusika (mipango miji na wapima), kuhakikisha watu wa namna hiyo wanashughulikiwa.

Pia aliwaonya wale wote wanaopitisha ramani (Wapima wa Mikoa) katika wizara kwa kuwaeleza kuwa hategemei siku tano mbele baada ya agizo hilo wapitishe ramani kinyume.

**■Habari hii ilichapishwa katika moja ya matoleo yaliyochapishwa mapema wiki hii kukiwa na matatizo ya kiufundi hivyo, tumeamua kuichapisha upya. Tunaomba radhi kwa usumbufu. - MHARIRI.**

# Mzee wa Upako apigia debe tozo

**Na Mary Geofrey**

MCHUNGAJI wa Kanisa la Maombezi la GRC, Anthony Lusekelo, maarufu Mzee wa Upako, amesema kanisa lake linaunga mkono makato ya kodi mbalimbali zinazotozwa na serikali kwa sababu ni kwa maendeleo ya taifa.

Vilevile, ameihimiza serikali kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kodi na manufaa yaliyopatikana ili wananchi wawe na utayari wa kuendelea kulipa.

Mchungaji Lusekelo alitangaza msimamo huo wa kanisa lake jana mkoani Dar es Salaam, ikiwa ni siku tatu tangu serikali itangaze kusikia kilio cha wananchi kuhusu tozo za makato ya benki na miamala ya simu na kuahidi kulifanyia kazi suala hilo.

Alisema suala la kodi halijaanza serikali ya awamu ya sita bali lilianza miaka mingi na hakuna taifa linaloweza kuendelea au kupiga hatua kama raia wake hawalipi kodi.

"Mgogoro kuhusu kodi, kuhusu tozo haujaanza leo, hata Yesu alikuta binadamu hatuna hulka ya kulipa kodi. Ili watu walipe kodi na uhuru, inahitajika elimu ya juu sana na wakati mwingine inahitajika nguvu na kutunga sheria.

"Njia za kutatua mgogoro wa kodi ni kuonyesha faida zake kama kujenga barabara, shule na kuwaonyesha wananchi juhudi hizo zimefanywa na wao, wapewe shukrani wananchi kwa kuambiwa," alisema.

Mzee wa Upako alisema kwa mataifa yaliyoendelea, yakiwamo ya Amerika na Ulaya, watu wanalipa kodi kwa hiari na ndiyo yanayosaidia mataifa ya Afrika katika miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Mimi ni kiongozi wa kiroho kwa miaka 40, nina uzoefu wa kutosha, watu hawataki kutoa sadaka, wanasema hawa viongozi ni 'wapigaji', hawataki kulipa kodi na hata kujenga makanisa kwa sababu yetu yalijengwa na Wajerumani," alisema Lusekelo.

Alisema mapato makubwa ya nchi za Ulaya na Amerika yametumika kujenga makanisa nchini na maeneo mengine.

Alisema kwenye biblia inaonyesha Wayahudi walifanya mgogoro wa kulipa kodi katika kujenga mji wao.

Septemba Mosi, mwaka huu, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akizungumza na waandishi wa habari Jijini Dodoma, alisema serikali imechukua maoni yote ambayo yametolewa na wananchi kuhusu suala hilo na italifanyia kazi na hivi karibuni itatoa tamko kuhusu utekelezaji wake.

Waziri huyo pia alisisitiza kuwa uamuzi wa kuweka tozo hizo ulifanyika kwa kushauriana na wananchi na faida za makusanyo ya tozo ni pamoja na ujenzi wa shule nchini kote.



Rais Mstaafu, Jakaya Kikwete, akiweka shada la maua, katika kaburi la aliyekuwa Mwandishi Mkongwe, marehemu, Charles Kizigha, aliyezikwa Boko, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ajali ya basi, fuso ilivyoua watu watano, kujeruhi 54

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WATU watano wamepoteza maisha huku 54 wakijeruhiwa katika ajali iliyohusisha basi na lori aina ya fuso yaliyogongana uso kwa uso eneo la Ibadakuli, Manispaa ya Shinyanga.

Ajali hiyo ikitokea majira ya saa nane usiku wa kuamkia jana wakati basi hilo likitoka jijini Dar es Salaam kwenda jijini Mwanza.

Basi lililopata ajali ni la kampuni ya Supernajimunisa lenye namba za usajili T 413 DAY na fuso lenye namba za usajili T 123 DJH lililokuwa linatoka Mwanza kwenda Dar es Salaam likiwa na mzigo wa dagaa. Baadhi ya majeruhi ambao walikuwa abiria katika basi hilo, wakisimulia namna ajali hiyo ilivyotokea, walidai kuwa walipokuwa njiani walilalamikia mwendokasi wa basi hilo.

Mmoja wa majeruhi hao, Fred Mahina, alisema dereva wa basi hilo ambaye bado hajafahamika jina, alikuwa akiendesha gari hilo kwa mwendokasi na walipokuwa wakimzuia, aliwajibu kwamba wangetaka usafiri wa raha, wangepanda ndege, huku akiwaambia waendelee kusali sana ili wafike salama.

"Tulipofika Morogoro, dereva akiwa mwendokasi alikwaruza lori, tukapona kuanguka, lakini akazidi kuendesha mwendokasi, abiria tulipokuwa tukipiga kelele apunguze mwendo, aligoma na kutuambia tusali sana ili tufike salama na tungetaka usafiri wa raha tungepanda ndege, na tulipofika hapa Shinyanga tumepata ajali," alilalamika Mahina.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Leonard Nyandahu, aliyekuwa eneo la tukio, alisema chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva wa basi kwa kutozingatia vibao vya usalama barabarani na kuendesha mwendokasi.

Alisema eneo ambalo ajali imetokea ajali, kuna kibao cha kuendesha mwendo wa kilomita 50, lakini dereva wa basi hakizingatia hilo na hivyo kusababisha ajali hiyo.

Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga, Dk. Luzila John, alithibitisha kutokea vifo vya watu watano hospitali hiyo kupokea majeruhi 54 ambao walikuwa wanaendelea na matibabu.

Alisema watu hao ambao wamepoteza maisha, bado hawajatambuliwa majina yao na wamehifadhiwa katika chumba cha maiti hospitalini huko.

# Waziri ateta na mabalozi Uingereza na Singapore

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amekutana na kufanya mazungumzo na mabalozi wa nchi za Uingereza na Singapore kwa nyakati tofauti kuhusu ushirikiano baina ya nchi hizo na Tanzania kwenye maeneo mbalimbali ya sekta ya nishati.

Mazungumzo hayo yalifanyika juzi katika ofisi za Wizara ya Nishati jijini Dar es Salaam, yakihudhuriwa na baadhi ya viongozi wa wizara na walioongozana na mabalozi hao.

Katika mazungumzo yake na Balozi wa Uingereza nchini, David Concar, Waziri January alijadiliana naye maeneo ya ushirikiano ambayo ni pamoja na kujengea uwezo wataalamu hususani katika kusasisha mpango kabambe wa kuendeleza sekta ya umeme nchini (Power System Master Plan), kubadilishana uzoefu katika eneo la umeme na katika utekelezaji wa miradi ya umeme wa nishati jadidifu.

Waziri Makamba aliwakaribisha wawekezaji wa Uingereza kuwekeza kwenye miradi ya ujenzi wa njia za kusafirisha umeme (Independent Transmission Providers) pamoja na miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia nishati jadidifu.

Balozi Concar alisema Serikali ya Uingereza ipo tayari kutoa msaada kwa Tanzania kwenye masuala ya kiufundi. Vivyo hivyo alisema serikali hiyo ina nia ya kushirikiana na Tanzania kwenye masuala ya nishati bora ya umeme wa kupikia (electronic cooking).

Wakati wa mazungumzo baina ya Waziri Makamba na Balozi wa Singapore, Daoglas Foo, walijadili kuhusu uwezekano wa Tanzania kununua mafuta kutoka Singapore na ushirikiano katika miradi ya nishati jadidifu.

Balozi Foo alimtaarifu Waziri January kuwa Serikali ya Singapore tayari imeshaanza kufanya mazungumzo na wafanyabishara wa Tanzania kwa ajili ya kuwa na makubalino ya biashara na kuongeza kuwa mwaka 2023, Singapore itatuma watalaamu wake Tanzania ili kujadili maeneo mbalimbali ya uwekezaji na ushirikiano.

# Taasisi yalia zebaki migodini

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

TAASISI ya Kuendeleza Wachimbaji Wadogo wa Madini nchini (FADev) imesema jamii ina jukumu la kuhakikisha wachimbaji wadogo wanasaidiwa ikiwamo kupewa elimu ili waachane na matumizi ya kemikali za zebaki kwa ajili ya kuosha mchanga wa dhahabu.

Katibu Mtendaji wa FADev, Theonestina Mwasha, alitoa rai hiyo juzi jijini hapa wakati akifunga mafunzo ya siku mbili yaliyohusisha wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari Kanda ya Ziwa pamoja na waandishi wa habari kwa lengo la kujadili na kuweka mkakati wa kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuboresha sekta ya uchimbaji mdogo wa madini nchini.

Alisema mafunzo hayo yatasaidia kuimarisha ushirikiano endelevu wa pamoja na namna bora ya kuandika habari zinazohusu sekta ya uchimbaji mdogo wa madini ili kuiboresha iwe na tija kwa taifa.

Alisema kundi hilo linatumia kemikali zebaki katika shughuli zake za kuosha mchanga wa dhahabu, jambo ambali ni hatari kwa afya ya binadamu na mazingira.

"Tunahitaji kulinda afya ya jamii dhidi ya madhara ya zebaki ifikapo mwaka 2025, hivyo wataalamu wa madini na ninyi wataalamu wa habari tunashirikishana na kubadilishana uzoefu, kwa pamoja tunaweza kuisaidia sekta ya uchimbaji mdogo, wachimbaji wadogo wamekuwa wakiharibu mazingira, lakini wakifundishwa watabadilika.

"Tumekuwa tukiwasaidia kupata huduma za kitaaluma na kifedha kwa kuwapa elimu na kuwaunganisha na taasisi mbalimbali za fedha kwa ajili ya kupata mikopo ili kujikwamua kiuchumi," alisema Mwasha.

Alisema wanaunga mkono jitihada za serikali katika kutekeleza programu za kubadilisha uchimbaji mdogo ili kutumia njia bora na salama ambazo zinalinda afya za wachimbaji wadogo pamoja na kutunza mazingira.

Meneja wa Miradi wa FADev, Evans Rubara, alisema dhamira ya taasisi hiyo ni kuwa na ushirikiano wenye tija na endelevu na waandishi wa habari pamoja na wahariri ili kusaidia kuikuza sekta ya uchimbaji mdogo wa madini nchini.

Alisema dira yao ni kuhakikisha shughuli za sekta ya uchimbaji mdogo wa madini ni adilifu, shirikishi na endelevu ili kuikuza sambamba na kuongeza stadi za maisha miongoni mwa wachimbaji.

Ofisa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Joseph Kiwango, akielezea mpango kazi wa taifa wa kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhababu, alisema matumizi ya kemikali hizo yanachangia athari mbalimbali zikiwamo magonjwa ya mifumo ya upumuaji, uzazi, neva, mishipa ya fahamu, figo, moyo, udhaifu na maumivu ya mwili, uchafuzi wa vyanzo vya maji na udhofishaji ukuaji wa viumbe hai wa majini.

Aliongeza kuwa harakati mbalimbali zinafanyika ili kukabiliana na athari za zebaki ikiwamo kuandaliwa kwa mpango kazi wa taifa wa kupunguza matumizi yake kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu.

Mpango huo pia unalenga kusimamia kanuni za udhibiti na usimamizi wa zebaki, kuaanda maandiko ya miradi pamoja na tathmini ya awali ya uwezo wa taifa kutekeleza mkataba wa Minamata ambao unazuia matumizi yake.

Mhariri wa Nipashe Kanda ya Ziwa, Richard Makore, alisema mafunzo hayo yatawasaidia kupata uelewa na kuwatembelea wachimbaji wadogo ili kusikiliza kero zao na kuziripoti.

Alisema jamii inaweza isielewe madhara yatokanayo na kemikali za zebaki, lakini yakitolewa mafunzo yatasaidia kupanua uelewa ili wachimbaji wadogo waachane na kuzitumia kwenye kazi zao.



Livia Mhagama (mwenye kipaza sauti) akijifunza kujinadi mbele ya wananchi jana, katika mafunzo yanayoendeshwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni jijini Dar es Salaam, kwenye Kata za Majohe na Kipunguni, ikiwa ni kampeni ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi za maamuzi, ambapo wanafundishwa namna ya kusimama majukwaani kuomba kura. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kinana aishukuru China ujenzi wa VETA Kagera

**Na Beatrice Shayo,** BUKOBA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Kanali mstaafu Abdulrahman Kinana, ameishukuru Serikali ya China kwa kufanikisha ujenzi wa Chuo cha Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) mkoani Kagera.

Mradi huo umegharimu Sh. bilioni 22 bila kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ambayo ilijumuisha katika shughuli za ujenzi, usimamizi na uwekaji wa vifaa vya kujifunzia, mashine na samani.

Kinana alitoa pongezi hizo jana baada ya kukagua chuo hicho, akiishukuru Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa kufanikisha ujenzi huo utakaosaidia Watanzania wengi kupata ujuzi.

"Ninaipongeza serikali kwa kazi nzuri inayofanya chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan katika sekta zote, ninyi ni mashahidi tangu Rais ameingia madarakani, shule nyingi zimejengwa, vyuo vingi vimejengwa na walimu wameajiriwa na wanafunzi wameongezeka.

"Nina hakika Watanzania wengi wataelimika, kwa hiyo ninampongeza Rais Samia kwa kazi nzuri anayofanya. Nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jamhuri ya Watu wa China, niishukuru Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, niseme bila kusita tunao marafiki wengi," alisema.

Aliwapongeza wananchi wa Bulugo kwa kutoa ardhi na ni matumaini yake kwamba wananchi hao watakuwa sehemu ya wanafunzi watakaosoma huko.

Kinana pia alikutana na kuzungumza na wanachama wa CCM Mkoa wa Kagera na kuwakumbusha viongozi kuwajibika kwa kuwatumikia wananchi na kusikiliza kero zao na kuzipatia ufumbuzi.

Alitumia nafasi hiyo kutoa maelekezo kwa viongozi wa mkoa huo kuhakikisha wanatatua kero za wananchi ikiwamo ya uuzaji wa kahawa baada ya kupokea malalamiko ya wakulima wa zao hilo kusumbuliwa na baadhi ya viongozi.

Kinana alishauri wakulima wa zao la kahawa waachwe wauze kahawa kokote wanakotaka kama bei ni nzuri.

# Wakulima 300 wakopeshwa zana za kilimo

**Na Paul Mabeja,** KONGWA

KATIKA kukabiliana na shida ya upatikanaji wa zana za kilimo nchini, Kampuni ya PASS LEASING imetoa mikopo ya vifaa mbalimbali kwa wakulima 300 vyenye thamani ya Sh. bilioni 16.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Killo Lussewa, alibainisha hayo jana wakati wa hafla fupi ya kuwakabidhi wakulima matrekta 15 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 500.

Alisema lengo la kuanzishwa kwa kampuni hiyo na serikali ni kutatua shida katika upatikanaji wa zana za kilimo kwa wakati kwa wakulima wadogo na wa kati nchini.

"Toka kuanzishwa kwa PASS LEASING mwaka jana hadi leo hii, tumewafikia wakulima takribani 300 na tumetoa vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh. bilioni 16 na katika mpango wetu wa miaka mitano hadi 2025, tunapanga kuwafikia wakulima 760 na kuwapatia zana mbalimbali za kilimo zenye thamani ya Sh. bilioni 32," alisema

Vilevile, alisema kabla ya kuanzishwa kwa kampuni hiyo, ilikuwapo Kampuni ya PASS ambayo ilikuwa na jukumu la kutoa udhamini wa mikopo kwa wakulima kuwafanya wakopesheke na kulima kwa tija.

Alisema kwa kipindi cha miaka 21, kampuni hiyo ilifanikiwa kuwafikia wakulima milioni 1.3 ambao walipatiwa udhamini wa mikopo yenye thamani ya Sh. trioni 1.3.

"Kwenye udhamini tulifanikiwa ndipo tukaona kuna shida katika upatikanaji wa zana za kilimo kwa wakati kwa wakulima wadogo na wa kati ndipo tukaamua kuanzisha kampuni hii ambayo imekuja kutatua shida ya vitendea kazi kwa wakulima," alisema na kuwataka wakulima nchini kuchangamkia fursa hiyo.

Alisema wajasiriamali 92 tayari wamewafikia jijini Dodoma na 48 wa Kongwa 48 na hadi sasa wameshatoa mikopo ya vifaa vya Sh. bilioni mbili na Kongwa peke yao wamepata Sh. bilioni 1.5.

"Niwaombe ndugu zangu mkope na kurejesha kwa uaminifu ili wengine nao wanufaike na fursa hii ya zana za kilimo ili walime kwa tija," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Mwema, akizungumza katika hafla hiyo, aliwataka wakulima kutumia fursa ya kilimo kuwekeza katika elimu kwa watoto wao.

Mwema alisema ni aibu kwa wakulima kukopa matrekta ya bei ghali lakini wakashindwa kuwapeleka watoto wao shuleni kuwapatia misingi imara ya elimu.

"Lazima mhakikishe watoto wanakwenda shuleni, hiki mnachokifanya sasa kinaweza kukosa maana kama watoto wenu watashindwa kwenda shuleni, pia itakuwa aibu watu kusema 'huyu mtoto ndiyo yule baba yake alikuwaga na matrekta mengi lakini alipofariki dunia, hali ikabadilika'. Lazima muwajenge msingi ya elimu watoto ili waendeleze hiki mnachofanya sasa hata kama hamtakuwapo," alisema Mwema.

Aliwataka maofisa ugani waliopatiwa usafiri wa pikipiki, kuhakikisha wanazitumia ipasavyo kuwatembelea wakulima na kutoa ushauri wa kitaalamu ili kuwasaidia kulima kwa tija na kujikwamua kiuchumi.

# Bil. 3/- zatolewa ujenzi wa shule ya sekondari

**Na Gideon Mwakanosya,** NAMTUMBO

SERIKALI imetoa Sh. bilioni tatu kutekeleza mradi wa shule ya sekondari ya wasichana ya Mkoa wa Ruvuma ambayo inajengwa katika eneo la Migelegele wilayani Namtumbo.

Akizungumza baada ya kukagua mradi huo jana, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, alisema ameridhishwa na utekelezaji wa mradi huo, shule hiyo ikitarajiwa kuanza kudahili wanafunzi mwakani.

Kanali Laban alisema Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa mikoa 10 ambayo serikali imetoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule maalum za sekondari za wasichana za mikoa.

"Mheshimiwa Rais anatafuta fedha kuhakikisha miradi mbalimbali inatekelezwa ukiwamo mradi huu wa sekondari za wasichana, ninawapongeza wote kwa kujitoa kusimamia kuhakikisha mradi huu unakamilika," alisema. Kanali Thomas alisema kuna baadhi ya mikoa inayotekeleza mradi huo haijaoiga hatua kubwa, lakini akawataka watekelezaji wa mradi huo mkoani m mwake kutobweteka badala yake kuhakikisha ujenzi unakamilika ndani ya mkataba.

Alitoa rai kwa wataalamu wanaosimamia mradi huo, kufanya kazi kwa uaminifu, weledi na kufuata sheria na kanuni, akiwaonya dhidi ya tabia ya udokozi wa fedha za miradi kwa kuwa watachukuliwa hatua.

Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Dk. Julius Ningo, aliahidi kusimamia kikamilifu mradi huo ili ukamilike kwa viwango na ubora unaolingana na fedha zilizotumika. Ofisa Elimu Halmashauri ya Namtumbo, Juma Fulluge, aliishukuru serikali kwa kupeleka fedha nyingi za ujenzi wa shule ya sekondari ya wasichana ya Mkoa wa Ruvuma.

Alisema katika awamu ya kwanza, zaidi ya Sh. bilioni 1.6 zimetolewa ambazo zimejenga vyumba 12 vya madarasa, mabweni matano, maabara tatu, vyoo na nyumba za walimu.

Alibainisha kuwa kazi inayoendelea kwa sasa ni ujenzi wa jengo la utawala na ukumbi wa shule, akitamba kuwa shule hiyo ikikamilika, itakuwa miongoni mwa shule bora mkoani Ruvuma.



Diwani wa Kata ya Kivukoni, Sharik Choghule, akiwa amembeba mtoto kwa ajili ya kuchanjwa Chanjo ya Polio katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam juzi. PICHA: JUMANNE JUMA

# RC aonya upotoshaji kuhusu chanjo polio

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, amewataka viongozi mbalimbali mkoani humo pamoja na wataalamu wa afya kuchukua hatua, ikiwamo kukanusha upotoshaji juu ya chanjo ya polio.

Kampeni ya utoaji chanjo hiyo kwa watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano ilianza kutolewa Septemba Mosi mwaka huu kwa nchi nzima na inatarajiwa kuhitimishwa leo na Mkoa wa Shinyanga unatarajia kuchanja watoto 445,681.

Mjema alitoa agizo hilo juzi wakati wa kikao cha kuhamasisha awamu ya pili ya chanjo hiyo mkoani Shinyanga.

Mkoa huo ulikuwa umepangiwa kuchanja watoto 349,007, lakini ulivuka lengo na kuchanja watoto 445,681 sawa na asilimia 128 na kuwa katika nafasi ya pili kitaifa.

"Chanjo hizi ni salama na zimethibitishwa na Wizara ya Afya pamoja na Shirika la Afya Duniani (WHO), hivyo niwaombe viongozi na wataalamu muendelee kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wa watoto kupata chanjo ya polio kupitia majukwaa mbalimbali.

"Tusipochanja watoto wetu chanjo hii ya polio, tutapata watoto wenye ulemavu na wasio na afya na taifa letu hapo baadaye litakosa wataalamu wakiwamo madaktari, hivyo tuhakikishe tunafikia malengo na kukanusha upotoshaji wowote dhidi ya chanjo hii," aliagiza.

Akizungumzia utoaji wa chanjo ya UVIKO-19, Mjema alisema katika mkoa huo hadi kufikia Agosti 31 mwaka huu, jumla ya watu 735,844 walikuwa wamechanja chanjo hiyo sawa na asilimia 73 na kuufanya mkoa huo kushika nafasi ya tano kitaifa.

Mratibu wa Chanjo mkoani Shinyanga, Timoth Sosoma, alisema dozi walizopokea za chanjo ya polio awamu ya tatu ni 492,000 na wanatarajia kufikia watoto 445,681 na hadi kufikia juzi, walikuwa wameshatoa chanjo hiyo kwa watoto 35,885.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Ushauri wa DC kuhusu mabadiliko sheria utumishi wa umma uzingatiwe

**MAKAMU** Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Kanali Mstaafu Abdulrahman Kinana, alifanya ziara mkoani Kigoma kwa ajili ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM kupitia miradi ya maendeleo inayofanywa na serikali na taasisi zake.

Katika ziara hiyo, Kinana alijionea miradi inayotekelezwa ikiwamo ujenzi wa bandari. Pia alifanya mikutano ya hadhara kadhaa ambayo wananchi waliitumia kutoa kero na madukuduku yao kuhusu masuala mbalimbali yanayowahusu.

Moja ya mambo yaliyoleta mwamko wa aina yake ni kauli ya Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Ester Mahawe, aliyeweka bayana kuwa kuna uozo wa kutisha serikalini. Alieleza mambo mbalimbali yanayofanyika katika serikali hasa ngazi za halmashauri ambazo ndizo watekelezaji wakubwa wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Mahawe aliweka bayana kwamba katika ngazi ya wilaya au halmashauri, wanaotupiwa jicho ni mkurugenzi na mkuu wa wilaya huku wakuu wa idara na vitengo, ambao ndio chanzo cha matatizo wakiwa hawaguswi kabisa.

Kutokana na hali hiyo, mkuu huyo wa wilaya alishauri kwamba panapotokea matatizo ndani ya halmashauri, mkurugenzi anapoondolewa, basi wakuu wa idara na vitengo wote waondolewe kwa sababu wote ni wahusika katika tatizo husika. Mahawe alisema hayo baada ya Kinana kuwataka viongozi kujibu hoja kuhusu kero zilizowasilishwa na wananchi katika mkutano alioufanya.

Alisema wazi kwamba watu wanafanya kazi kwa mazoea,. Hivyo kukwamisha utekelezaji wa masuala mbalimbali ya maendeleo. Hali hiyo, kwa mujibu wa Mahawe, inatokana na watu hao kuamini kwamba hata wasipofanya kazi kwa ufanisi na kujituma, wataendelea kupata mishahara na hakuna wa kuwagusa kwa kuwa mikataba yao ya kazi ni ya kudumu, kwa maana kwamba hawawezi kuondolewa hadi kustaafu kwao.

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, aliishauri serikali kufanya mabadiliko ya sheria za utumishi wa umma kwa kufuta mikataba ya kudumu na kuanzisha mikataba ya muda maalum. Alitolea mfano wa sekta binafsi alikofanya kazi kabla ya kuteuliwa kuwa mkuu wa wilaya kuwa huko kuna mikataba maalumu ya ajira, hivyo kinachoangaliwa ni uwezo na umahiri wa mtu katika utendaji kazi.

Wazo hilo la kuwapo kqwa mikataba maalumu ni jema kwa sababu serikali imekuwa ikihimiza weledi na kufanya kazi kwa bidii na kuleta matokeo chanya katika utumishi wa umma pamoja na watumishi kujiepusha na uvivu, wizi na rushwa katika kutekeleza majukumu yao.

Ni imani kwamba kuwapo kwa mikataba maalum ya kazi, kama ilivyo kwa mashirika ya kimataifa, baadhi ya taasisi za serikali zikiwamo wakala na mamlaka na sekta binafsi, kutaongeza nidhamu katika utendaji kazi. Hii haimaanishi kuondoa mamlaka za uteuzi kwa Rais bali wahusika watateuliwa kwa kuangaliza sifa na vigezo lakini kazi zao zitakuwa za mikataba maalum.

Hatua hiyo pia itapunguza visingizio na sababu zisizo za msingi kwa watumishi wakiwamo wakuu wa idara, wakurugenzi na wakuu wa wilaya pamoja na makatibu tawala kutokana na kukosekana sehemu za kazi. Kuwapo kwa sheria inayohusu mikataba maalum kutasaidia watu kujituma kwa sababu watatambua kuwa kuendelea kwao kutatokana na utendaji kazi wao na si vinginevyo.

Ni vyema ushauri huu ukazingatiwa na kufanyiwa kazi haraka ili sheria ya utumishi wa umma ibadilishwe na hatimaye kuwekwa vipengele vitakavyowabana watumishi ambao wamekuwa mzigo na kusababisha serikali kulaumiwa kila uchao. Pia ni muhimu ushauri wa kutimua watendaji wote katika halmashauri ukazingatiwa badala ya kutimuliwa wakurugenzi pekee huku wakuu wa idara na vitengo wakiendelea kwenye utumishi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Sabato Kasika

### Fursa hizi za elimu kwa mwanafunzi wa kike si za kukosa

**KATIKA** Kiswahili, kuna msemo kwamba ukielimisha mwanamke, umeelimisha jamii nzima. Msemo huo unalenga kuhamasisha elimu kwa mtoto wa kike ambaye miaka ya nyuma alikuwa hapewi kipaumbele kwenye elimu.

Uhamasishaji huo wa elimu kwa mtoto wa kike umekuwa ukifanyika kwa njia mbalimbali ikiwamo kuwarudisha shuleni wale ambao kwa bahati mbaya walipata ujauzito kabla ya hawajahitimu masomo yao.

Vilevile watoto wa kike pia wamekuwa wakihamasishwa kupenda masomo ya sayansi ambayo kwa miaka mingi yalionekana kuwa ni ya wanafunzi wa kiume tu, kana kwamba wao hawawezi kuyasoma.

Kinachoendelea sasa katika elimu kwa ajili ya watoto wa kike, ni wazi hawana budi kuitumia fursa hiyo vizuri ili waweze kufaidika kielimu, huku wakitambua kuwa mwanamke mmoja akielimika, jamii nzima itakuwa imeelimika.

Kwa mfano, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) umekuwa ukitoa mafunzo ya kuhamasisha mtoto wa kike kupenda masomo ya sayansi, kuwa mbunifu na kupenda kujifunza masuala ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Mfuko umekuwa ukitekeleza mradi wa kutoa vifaa vya TEHAMA kwa shule za umma na kusaidia katika kuziunganisha na mtandao wa intaneti, ili kurahisisha mchakato wa kujifunza masomo ya teknolojia hiyo.

Hizo ni fursa muhimu ambazo zinaweza kuwafanya watoto wa kike kupata elimu na kuwa na ujuzi ambao watautumia kwa ajili ya maisha ya baadaye wanapohitimu elimu katika ngazi mbalimbali.

Hivyo kwenye suala la TEHEMA, ni vyema kutambua kuwa ubunifu si kwa ajili ya mtoto wa kiume bali ni kwa wote, ambao wanapenda kupata ujuzi na ubunifu wa vitu mbalimbali kupitia masomo ya sayansi.

Mtaalam mmoja wa saikolojia, Roselight Ringo, anasema mtoto wa kike akielimika, anakuza uwezo mkubwa wa kufikiri kwa umakini na uyakinifu, na kwamba uwezo huo ndio unaohitajika katika jamii ya leo.

Katika ufafanuzi wake, anasema mtu mwenye uwezo wa kufikiri ndiye mwenye nguvu ya kuibua dhana mpya, kutafuta njia mbadala za kutatua matatizo na kuelekeza wenzake katika matendo sahihi.

Anaongeza kuwa uwezo huo ndio unaomwongoza kila siku katika utendaji wake, na kwamba wanawake wenye elimu ndio wanaojitambua na kujimiliki wenyewe kwanza, kuzikabili changamoto zinazowasonga.

Lakini pia anabainisha kuwa kumsomesha mwanamke, kunachangia kwa asilimia kubwa kuokoa uhai wa watoto wengi, kupunguza utapiamlo na kupunguza vifo vya watoto kwa asilimia kadhaa.

Kwa nini? Anasema kwa sababu mwanamke aliyesoma anaweza kuwa mama wa watoto anayejua kanuni za afya, lishe bora ya mtoto na uzazi bora, na kwamba atailinda afya ya familia yake dhidi ya maradhi.

Pamoja na hayo anasema mwanamke aliyesoma anafahamu njia za kujikinga, ana uwezo wa kufanya uamuzi kuhusu mwili wake, na hata kuwa makini kuhusu uhusiano wake na mwanaume.

Ninaungana na mtaalam huyo, kwani kupitia elimu, mtoto wa kike angeweza kuyatawala na kuyatumia mazingira yanayowazunguka ili kuboresha maisha yake, kujua haki zake na wajibu wake.

Hivyo wakati huu ambao serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu inaweka mikakati ya kuinua elimu ya mtoto wa kike, walengwa wangelitambua hilo na kulifanyia kazi.

Ikumbukwe kuwa kila mara imekuwa ikizungumzwa kuhusu umuhimu wa wazazi na jamii kuwapa watoto nafasi sawa ya kupata elimu bila kujali jinsi, hiyo inatokana kwamba watoto wa kike hawatakiwi kubaguliwa.

Juhudi zote zinazofanywa na serikali hadi kufikia kuweka mkakati wa kuwarudisha shuleni wale wanaopata mimba kabla ya kuhitimu, zinaonyesha ni jinsi gani elimu ilivyo muhimu kwa jinsi zote.

Hatua hiyo pia ingefaa kusaidia jamii kuachana na dhana potofu ya kuamini kuwa mtoto wa kike hawezi kufanya kitu cha muhimu ukilinganisha na wa kiume, kwani dhana hiyo inatokana na mfumo dume uliotawala katika jamii.

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Tuijue EAC na fursa zake kwa maendeleo endelevu



Na Pascal Mayalla

**Mtangamano umeainisha kabla ya kuunda shirikisho, hatua ya kwanza inayopaswa kufanywa ni kuunganisha baadhi ya mambo na kuwa na kitu kimoja ndipo ifikie hatua ya kuwa nchi moja.**

SAFU hii 'Kwa Maslahi ya Taifa', inakuletea mfululizo wa makala za kuelimisha Watanzania kujua Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ambao ukikamilika, utaunda taifa kubwa kabisa la Afrika Mashariki ambalo litakuwa na serikali moja ya Afrika Mashariki.

Taifa hilo litakuwa ndilo taifa kubwa la nne duniani, baada ya Marekani, China na Russia. Kati ya nchi zote saba za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania ndiyo inayoongoza kwa fursa nyingi lakini kwa bahati mbaya sana, Watanzania hawajui na hawazichangamkii, hivyo ni bora wakafufuliwa macho na hatimaye kuzichangamkia.

Kuelekea mtangamano wa Afrika Mashariki, mchakato huu unazihusisha nchi saba za Ukanda wa Maziwa Makuu zenye utajiri mkubwa wa madini, maliasili, vyanzo vya maji, udongo wenye rutuba na mtangamano ukikamilika na kuwa nchi moja, hakuna nchi nyingine yoyote barani Afrika, inaweza kushindana na utajiri huu.

Nchi hizo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Sudani Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na zina eneo la kilomita za mraba 4,810,363 na wakazi 281,050,447 kwa kadirio la mwaka 2022. Kwa maana hiyo tangu awali ingekuwa nchi moja tu, ingekuwa ya nne duniani, ikipitwa na China, Marekani na Russia pekee.

Kwanza kabisa, niwaelimishe kuhusu Mkataba wa Kuanzishwa Upya kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliotiwa saini Novemba 30, 1999 na kuanza kutumika rasmi Julai 7, 2000 baada ya nchi washirika watatu wa mwanzo, Tanzania, Kenya na Uganda kuridhia.

Mkataba huo uliazimia kuziunganisha nchi washirika za mwanzo, Tanzania Kenya na Uganda kuwa nchi moja kupitia mchakato unaoitwa mtangamano ambao unakwenda hatua kwa hatua hadi kufikia kuwa na shirikisho la nchi moja.

Mtangamano umeainisha kabla ya kuunda shirikisho, hatua ya kwanza inayopaswa kufanywa ni kuunganisha baadhi ya mambo na kuwa na kitu kimoja ndipo ifikie hatua ya kuwa nchi moja.

Hatua ya kwanza ni kuunda vyombo, sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuwa na pasipoti moja, viza moja ya watalii, muungano wa sarafu, na mwisho ni shirikisho la kisiasa.

Maeneo hayo kujenga mfumo kamili wa ushirikiano katika biashara, uwekezaji na maendeleo ya viwanda; sarafu na sera za fedha, miundombinu na huduma, kilimo na uhakika wa chakula, mazingira na usimamizi wa maliasili; utalii na usimamizi wa wanyamapori.

Nyanja zingine za ushirikiano zilizoainishwa katika mkataba ni shughuli za afya, kijamii na kiutamaduni; nafasi ya wanawake katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi, ushirikishwaji wa sekta binafsi na jumuiya za kiraia; pamoja na ushirikiano katika masuala ya sheria na utoaji haki: masuala ya kisiasa ikiwa ni pamoja na ulinzi, usalama na mambo ya nje.

Mkataba pia unaeleza hatua mbalimbali katika maendeleo ya mtangamano ukiwamo uanzishaji wa muungano wa forodha, ambao ni mlango muhimu katika shughuli za jumuiya, kisha baadaye soko la pamoja likifuatiwa na muungano wa sarafu na hatimaye shirikisho la kisiasa la Dola la Afrika Mashariki.

Mkataba huo umetilia maanani maslahi ya eneo hili la Afrika Mashariki. Inaeleweka kwamba mataifa madogo na dhaifu hayana mustakbali murua katika ulimwengu huu wa ushindani mkubwa.

Kwa kuwezesha kuwapo kwa soko pana zaidi, jumuiya itasaidia kukuza biashara na uwekezaji katika eneo hili.

Ushirikiano katika kukuza sayansi na teknolojia utatusaidia kwenda na wakati na kuongeza kasi ya ukuaji viwanda na hivyo kuongeza ajira na kuboresha hali za maisha ya watu.

Kwa ujumla, jumuiya itatuongezea fahari, hadhi na kujiamini, tena itaboresha nafasi yetu katika mahusiano na jamii nyingine duniani. Uelewa mzuri wa Jumuiya hii ndiyo mwanzo wa Watanzania kushiriki kikamilifu na kuchangamkia fursa za Mtangamano katika eneo letu hili. Ili kuwa na uelewa mpana, Watanzania wanapaswa kuhabarishwa na kuelimishwa kuifahamu EAC na fursa zake ili wazichangamkie na kuzifaidi.

Historia, iliyopo sasa inayozihusisha Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Sudani ya Kusini na DRC, ni ya pili. Jumuiya ya kwanza ilinzishwa mwaka 1967 ikizihusisha nchi tatu tu za Tanzania, Kenya na Uganda, makao makuu ya jumuiya yakiwa Arusha, Tanzania. Kwa bahati mbaya sana, Jumuiya hiyo ilivunjika mwaka 1977.

Tukutane wiki ijayo, ili kujua kwa nini jumuiya ya kwanza ilivunjika ili kuzitumia sababu hizo kuzuia hii jumuiya ya pili nayo isije kuvunjika kama ile ya mwanzo.

**Wasalaam**
**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tusibonyeze mguu wa majeruhi kujua unaumaje!



Na Joseph Kulangwa

**Jirani yangu hapa Mbagala Kizuiani aliniuliza:" Eti jirani nataka kwenda Morogoro ambako nauli ni Sh 10,000, nikitaka kutoka hapa nyumbani nikapande mabasi Mbezi kwa Magufuli kwa teksi sharti niwe na si chini ya Sh 50,000.**

JE, uliwahi kusikia wimbo huu? "Pesa ni kitu kidogo hapa duniani eh, lakini mateso yake yamezidi kiasi eh! Watu wengi wamepoteza maisha yao oh, sababu ya kitu kidogo kiitwacho pesa! Unasafiri kwenda nchi za ng'ambo eh, sababu ya kitu kidogo kiitwacho pesa.

"Ndugu na ndugu huweza hata kuuana eh, sababu ya kitu kidogo kiitwacho pesa! Oh ni kitu gani eh, pesa pekee ndiyo itusumbuayo ooh!..." Huu ni wimbo wa bendi maarufu iliyowika nchini miaka ya sabini. Ikijulikana kama Afro 70 ikipiga mtindo wa Afrosa.

Wimbo huu unaakisi hali ilivyo nchini hivi sasa. Kila kitu kinategemea pesa, vilio vingi vya wananchi ni pesa, ukigeuka huku ni tozo, ni kodi, ni ushuru na mambo mengine kama hayo. Watu wanaambiwa tozo na kodi ndiyo maendeleo hawaelewi, kwa sababu mifukoni hakuna pesa.

Wakati hayo yakiendelea, kuna watu wanatazama ni jinsi gani waibe, wajibiie na au waliibie taifa ili kila siku mifuko yao iwe na pesa, ndiyo sababu Patrick Balisidya na wenzake wa Afro 70 wakasema ndugu na ndugu huweza hata kuuana, sababu ya kitu pesa.

Wizi na ubadhirifu katika taasisi za umma na hata binafsi umekuwa wimbo wa kawaida kabisa, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), anakagua na kuja na mapendekezo na hatua zinakaribia au zinachukuliwa, lakini watu bado wanaiba tu hicho kitu kidogo pesa.

Angalia serikali nayo inavyokuna kichwa kila siku kutafuta vyanzo vya pesa mpaka inafikia kuweka tozo kwenye miamala. Inafanya kila kitu ili hatimaye pesa ipatikane, miradi ya kimkakati na isiyo ya kimkakati inajengwa na kutekelezwa. Yote hayo ni nguvu ya kitu kidogo pesa.

Lakini wakati mwingine unashangaa kuona kama mchezo kwani daktari anaona kabisa majeruhi wa ajali ya bodaboda amevunjika mguu, bado anamminya pale pale palipovunjika, huku akimwuliza majeruhi kama panauma!

Hivi kweli pasiume wakati pamevunjika? Huo utakuwa mwili au jabali lisilosikia uchungu na maumivu? Ni kama ilivyo hivi sasa, tunaweka tozo kila mahali na tunaona kabisa zinaumiza wananchi hata wanaoweka fedha zao benki zinakatwa mara mbili, kuingia na kutoka, halafu tunauliza panauma, huku tunaminya kidonda!

Tunapoweka tozo halafu baada ya muda tunasikilizia wananchi wakilia maumivu na kisha tunasema tumekusikieni ngoja tufanyie kazi, kweli ni sawa hiyo? Hatuoni tunazidi kubonyeza mguu ulipokatika wa dereva bodaboda kweli?

Tunazuia mabasi kupakia kwenye stendi za binafsi tukitaka kila anayetaka kusafiri sharti aende stendi ya Magufuli, Mbezi Luis, bila kujali umbali anaotoka, kweli si kuminya mguu wa majeruhi na kumwuliza kama unauma kweli?

Jirani yangu hapa Mbagala Kizuiani aliniuliza:" Eti jirani nataka kwenda Morogoro ambako nauli ni Sh 10,000, nikitaka kutoka hapa nyumbani nikapande mabasi Mbezi kwa Magufuli kwa teksi sharti niwe na si chini ya Sh 50,000. Huo kama si wendawazimu ni nini? Halafu tunazuia mabasi kisha tunawasikilizia wananchi walie kwanza, ndipo tuseme tunalifanyia kazi!

Tukaanzisha bima ya afya na kuweka watu wa kuisimamia tena kwa nia njema kabisa, tukiamini kwamba afya ni kila kitu katika maisha ya binadamu ambao ni nguvukazi ya Taifa, na bila wao hata hii miradi tunayotambia leo, haiwezi kufanyika, lakini kwa kuwa tunajua kitu pesa ni kidogo lakini kigumu, basi bima hiyo hapo.

Waliopewa kusimamia nao kwa ujanja ujanja wanaanza kuinajisi kwa kushirikiana na watu kuiibia bima yenyewe isiyo na bima ya wizi. Mfuko unalegalega, tunawajua wezi, lakini tunataka ufe kwa ubozi wetu tu na sijui kwa faida ya nani, badala ya kuwalambisha sumu wanaotaka kuua Mfuko wetu!

Waziri Ummy Mwalimu bila shaka inamwuma sana kuona mtoto anataka kumfia mikononi, hivyo hana jinsi ila kupambana bima ya afya kwa wote ije, lakini ajue pia kuwa hata ikija, pesa ni kitu kidogo lakini mateso yake yamezidi kipimo. Kabla hajawasilisha muswada wa sheria ya bima kwa wote, afikirie kiwango cha pesa.

Hivi mathalan kila mtu akilipia Sh 10,000 kwa mwezi, hatutatibiwa kweli? Kwa sababu pamoja na kwamba magonjwa yasiyoambukiza ndiye chunusi la fedha zetu, hivi hata watu milioni 40 tukilipa hicho kiwango kila mwezi Mfuko utakufa kweli? Hapana, tujifikirie huku tukiacha kufanya mambo kwa majaribio, kwani tozo, stendi Magufuli na Bima ya Afya ni kama tulikuwa tunajaribu kubonyeza mguu wenye majeraha. **Alamsiki!**

# Mtumishi adaiwa kunaswa na rushwa

**Na Beatrice Shayo,** BUKOBA

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, amesema ndani ya saa tatu wamemkamata mtumishi wa serikali akiwa amejiingizia rushwa ya Sh. 960,000 na orodha ya wengine 14 inatarajiwa kuanikwa kesho.

Chalamila alibainisha hayo jana baada ya Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Kanali mstaafu Abdulrahman Kinana, kutaka serikali kutafakari upya suala la utoaji wa leseni za biashara hasa kwa watu wanaoanza biashara.

Kinana yuko mkoani Kagera kwa ziara akiambatana na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Shaka Hamdu Shaka, kwa ajili ya ukaguzi wa uhai wa chama, utekelezaji wa ilani na kusikiliza kero za wananchi.

Chalamila alisema kuna baadhi ya watumishi wa serikali wanapindisha sheria kwa kujitengenezea mazingira ya rushwa.

"Kuna mfanyakazi mmoja ameonekana ndani ya saa tatu amelipwa Sh. 960,000 kama rushwa na wengine 14 mpaka Jumatatu jioni utaipata taarifa yao, hatutaki kuona wananchi wanawekewa sheria ngumu ili wao wapate rushwa," alisema Chalamila.

Kiongozi huyo alisema malalamiko yaliyotolewa kuhusu suala la mageti ya vizuizi vya ushuru mara nyingi yamekuwa chanzo cha fedha za wala rushwa na kutumika kuwanyanyasa watu.

"Makamu Mwenyekitu huu mkoa una vizuizi vingi, ni mchwa wa maendeleo, wanachukua vitu vya watu mpaka mikungu ya ndizi, kesho yake unakwenda kufuatilia haipo, ukiuliza haupewi majibu ya kueleweka, wanawanyanyasa hawa wananchi ili kupata rushwa," alisema Chalamila.

Alisema tayari ameshaanza kuchukua hatua kwa kuunda kamati ndogo ili baadhi ya mageti ya ushuru yapunguzwe kwa kuwa hata yeye alishaona ni kero kwa wananchi.

Alisema kuna shida kwenye makusanyo ya mapato katika maeneo yote ikiwamo baadhi ya wafanyakazi wa Mamlaka ya Mapato (TRA) wanaovitumia vituo vyao vibaya kwa kutoza faini kubwa kwa wasafirishaji na kusababisha mhusika kutafuta njia mbadala na hata kutoa rushwa.

Alisema yupo mfanyakazi wa TRA wameanza kumsaka amekuwa akitoa maelezo ya kukataa maelekezo ya serikali kuhusu utaratibu wa sheria unaotakiwa kufuatwa.

Awali Kinana aliwashauri wabunge kuangalia sheria hizo kandamizi kwa kuwa kazi ya kurekebisha sheria ni yao lakini wamekaa kimya wakiachia wataalamu ambao hawaishi na wananchi.

"Utakuta mtu ana mtaji wa laki mbili lakini anatakiwa leseni, sasa atakavyozungushwa, malipo na urasimu wake utakuta laki mbili zimekwisha na hana fedha tena, sijui nini maana yake," Kinana alisema.

Mbunge wa Bukoba Vijijini (CCM), Dk. Jason Rweikiza, alisema mbali na wingi wa mageti ya ushuru, wana malalamiko kwa wakulima wa zao la vanila wa Mkoa wa Kagera ambao waliuza bila kulipwa fedha zao mwaka jana.

Dk. Rweikiza alimwomba Kinana kumsaidia kilio hicho kwa sababu kimekuwa cha muda mrefu bila majibu.



Kiongozi wa Kanisa la Maombezi la GRC lililopo Ubungo- Kibangu jijini Dar es Salaam, Anthony Lusekelo, maarufu 'Mzee wa Upako' akizungumza na waandishi wa habari jijini humo jana kuunga mkono juhudi za Serikali za kukusanya Kodi kupitia miamala mbalimbali kwa wananchi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Tanzania yajizatiti kukabili mabadiliko ya tabianchi

**Na Pilly Shaban**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, amesema azma ya serikali kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi iko pale pale na ndiyo maana inafanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha shida hiyo inapata suluhisho.

Alitoa kauli hiyo juzi jijini Dar es Salaam wakati akifunga Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi na Maendeleo ulioandaliwa na Serikali ya Tanzania kwa ushirikiano na Serikali ya Uingereza.

Balozi Mulamula alisema Tanzania imetimiza wajibu wake katika mapambano dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi ambapo miongoni mwa jitihada zilizofanyika ni kuzindua Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021.

Alisema katika Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi na Maendeleo mambo mbalimbali yamejadiliwa ikiwamo nchi zinazoendelea kukumbushwa kutimiza ahadi zao za kutoa fedha kwa ajili ya kusaidia katika harakati hizo.

Balozi Mulamula alikumbusha kuhusu ahadi zilizotolewa katika Mkutano wa COP 26 Novemba 2021 Scotland za kusaidia Tanzania na nchi zingine zinazoendelea katika kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kusema ni wakati sasa wa utekelezaji.

"Ninaamini kwamba siku hizi mbili za mkutano zimekuwezesha kutoa mchango mkubwa katika kurahisisha upatikanaji wa fedha za mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. Ninaamini pia mkutano huu utakuwa ni mwanzo wa ushirikiano bora kwa mataifa mbalimbali," alisema.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Omar Dadi Shajak, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) katika bajeti ya mwaka 2022/23 imetenga Sh. bilioni 4.1 kwa ajili ya mapambano dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema Visiwa vya Zanzibar vinakabiliwa na athari hizo katika maeneo yote na hivyo kuathiri shughuli za kilimo ambapo majichumvi yanaingia katika mashamba ya mpunga. Dk. Shajak alisema kuwa ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi na Maendeleo utasaidia katika kuja na suluhu ya shida hizo za mabadiliko ya tabianchi kwa upande wa Zanzibar.

Mkutano huo uliofunguliwa Septemba Mosi mwaka huu na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, ni maandalizi ya Mkutano wa 27 wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP27) unaotarajiwa kufanyika Misri Novemba 2022.

## Serikali yazindua kampeni usafishaji bahari na maziwa

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Suleiman Jafo, amezindua kampeni ya usafi wa visiwa vya Bahari ya Hindi na maziwa utakaohusisha kuondoa taka chini ya maji.

Kampeni hiyo ilizinduliwa jana Wilaya ya Kigamboni mkoani Dar es Salaam baada ya wazamiaji kufanya usafi chini ya bahari katika Kisiwa cha Mwakatube, kikiwa ni miongoni mwa visiwa vitatu vilivyoko wilayani huko.

Akizungumza baada ya usafi huo kufanywa na wazamiaji zaidi ya 20, wageni wakiwa watano waliokwenda chini ya Bahari ya Hindi mita 25, Waziri Jafo alisema tukio hilo ni la kwanza na la kihistoria kufanyika ambalo litawezesha kutunza mazingira na kukuza uchumi kupitia utalii.

Kupitia kampeni hiyo ijulikanayo 'Usafi wa Mazingira, Tunza Mazingira', wazamiaji hao wameweza kuondoa taka mbalimbali kwenye miamba chini ya baharini zikiwamo chupa za plastiki, mifuko ya pastiki na nyavu za wavuvi.

Jafo alisema Kisiwa cha Mwakatube kina urefu wa kilometa za mraba 7.78 ambacho ni fursa ya kiuchumi na utalii na kuielekeza Wilaya ya Kigamboni kukitangaza ili kipate mwekezaji wa kukiendeleza.

"Uchumi wa buluu tunaweza kuufanya Tanzania, eneo lile linaweza kufanya utunzaji mazingira na utalii, ikiwezekana leo ikawe ajenda rasmi kukitangaza tutafute mwekezaji mzuri.

"Kukitengenezwa vibarabara kwa ajili ya kukimbia na mbio za baiskeli na hapa eneo la Mikadi kukatengenezwa gati, inawezekana watu watafika mamia kwa mamia kwenda kule kisiwani," alisema.

Waziri Jafo alisema Tanzania ina visiwa vingi lakini hawajajielekeza katika kuvifanyia usafi, hivyo kupitia kampeni hiyo iliyozinduliwa, anaamini vitafikiwa vyote na kutangazwa.

Waziri huyo pia amepiga marufuku shughuli zote za uchimbaji mchanga kwenye fukwe za Bahari ya Hindi zinazofanywa ambazo zinachangia uharibifu wa mazingira.

Marufuku hiyo ilitolewa na Dk. Jafo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa Mkurugenzi wa Mikadi Adventure iliyopo Kigamboni, akilalamikia baadhi ya watu wamekuwa wakifanya shughuli hizo na kusababisha fukwe kulika na maji.

"NEMC (Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira) fanyeni ufuatiliaji, ninajua ofisi ya mkuu wa wilaya imeanza kulifanyia kazi shirikianeni.

"Lipo suala lingine la kelele na mitetemo, wote wenye kumbi za starehe wapige muziki katika viwango vinavyokubalika, atakayekiuka hilo amevunja sheria," Dk. Jafo aliagiza.

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Fatuma Nyangasa, alisema wilaya imekuwa na utaratibu mzuri wa kuviangalia na kuvifanyia usafi visiwa vilivyopo humo kwa kushirikisha taasisi mbalimbali.

"Tunahakikisha vinafanyiwa usafi na kuangaliwa kwa sababu kuna uhifadhi mkubwa ndani ya visiwa hivyo, ni visiwa ambavyo vinaweza kutumika vizuri kwa manufaa ya uchumi wa Kigamboni na kwa taifa kwa ujumla," alisema.

Mwandaaji wa kampeni hiyo, Balozi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, Richard Kalongola, alisema ameshirikisha wataalam wenzake wa maji kuja na kampeni hiyo ya usafi itakayohusisha kuondoa uchafu chini ya bahari.

"Kampeni imezinduliwa, tutaunda kamati maalum ya kitaifa chini ya ridhaa ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na baadhi ya mabalozi na wakazi wa visiwa husika kuhakikisha hatutupi taka wala kuchafua mazingira," alisema.

# MAISHA

SEPTEMBA 4, 2022
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
*Jumapili*




Ukurasa 14


## Jinsi ya kukaanga chapati laini



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Tunza mazingira nyumbani kama ni mfugaji wa mbwa




## KATUNIKA


Ukurasa 16




# Bangili za vifuu zinavyonogesha urembo

Ukurasa 14

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | D | I | M | B | A |
| ■ | O | ■ | ■ | A | ■ |
| O | N | A | ■ | M | ■ |
| ■ | Y | ■ | I | B | A |
| ■ | O | ■ | ■ | I | ■ |
| Y | A | N | G | A | ■ |

## AMSHA AKILI

TAU KALETEWA ZAWADI, MSAIDIE AIPATE



## TOA TOFAUTI 5




## WATOTO

# PAKA RANGI




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
INA, MWA, SAUMU, LAANA, NYUNGU, LAWAMA

## CHEKA



### Alichokifanya daktari

MTOTO Heri alikuwa akilima bustani ya mboga na bibi yake.

Wakati wakiendelea na kazi ya kuondoa magugu, bibi yake alikuwa akimsimulia jinsi ya kutengeneza majembe ya mkono.

Bibi: Ukitaka kutengeneza jembe la mkono lazima chuma ukifue kwa moto ili kilainike.

Heri: Sawa bibi, lakini mwalimu alituambia eti jembe haliwezi kumtupa mkulima, ni sawa?

Bibi: Ndio mara nyingi mkulima anategemea mavuno mazuri

Heri: Sasa kama likimtupa, mkulima hapati mazao?

Bibi: Huo ni msemo tu wa kumpa moyo mtu anayefanya kazi kwa jasho lake, lakini huwa anakosa mavuno kutokana na sababu mbalimbali.

SWALI
Vijiti vinavyotumika kuwasha moto kwa kusugua vinaitwaje?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Masharti ya waganga wa jadi yalivyoua utajiri wa Selestine

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na kisa cha kijana Selestine aliyedhani waganga wa jadi wangemtajirisha, matokeo yake akawa masikini wa kutupwa. Kwa wasomaji wanaofuatilia kisa hiki, hii ni sehemu ya nne na pengine inaweza kuendelea hadi sehemu ya tano.

Ni kisa cha kitisha, chenye fundisho kubwa sana hasa kwa vijana wanaoshindwa kumtumainia Mungu ambaye ni muweza wa vyote, badala yake wanakimbilia kwenye nguvu za giza. Mungu mwenyewe anasema katika amri zake "Usimwabudu Mungu mwingine ila mimi". Pia anasema "na alaaniwe mtu yule anayemtegemea mwanadamu kuwa kinga yake". Wiki iliyopita tuliishia pale Selestine akiwa ndani ya pango anakoishi joka kubwa alikopelekwa na mganga. Ilikuwa alambwe kiganja cha mkono na joka hilo kama ishara ya kusalimiana lakini alikataa. Adhabu yake akatozwa faini Sh.500/= Akaomba msamaha, akaweza kutoka mle pangoni na mganga wake.

Baada ya kutoka kwenye pango, anasema; sikwenda tena kwa mganga ila alinipatia masharti yafuatayo;- kwamba nikifika nyumbani nisisalimiane na mtu yoyote na asubuhi nikanunue ndoo tatu nisitie ndani kitu chochote na siku ya nne nikifungua nitakuta fedha. Lakini fedha hizo nisizitumie kabla ya kutoa Sh.50,000/= kwa wahitaji. Na sharti la tatu ikitokea mitaani kwetu kuna msiba, mgonjwa au harusi nitoe gharama zote na nisipofanya hivyo fedha yote itayeyuka. Na kweli nilipofungua ndoa nikakuta humo Shilingi milioni mbili.

Nakumbuka siku moja ya Jumapili niliienda kusali, padre mmoja Mjerumani akiwa na kawaida ya kusalimiana na watu, baada ya misa kuisha nilimpa mkono kumsalimia akasema nisimame pembeni. Baadaye akaniambia kuwa mimi nina kitu, tena nguvu za giza, hivyo niende nikazitoe na kuzitupa au kuzichoma.

Nikamwambia ndani kwangu nina ndoo tatu tu. Padri akasema ndoo hizo zina kitu ila wewe hukioni. Alipoona nimesita akaniambia wewe hukioni kilichomo ndani yake na kama huamini twende sasa hivi mimi nikakitoe.

Hapo nikaishiwa nguvu kwani masharti yananipasua kichwa. Katika fedha nilizokuta kwenye ndoo, nikachukua kama shilingi milioni moja na nusu kununua choroko.

Nikaenda kwa mkulima akaniambia gunia moja ni Sh. 50,000. Nikaomba apunguze hadi sh. 40,000. Nikamwambia hayo magunia 10 nitayachukua yote. Ikabidi nikachukue mifuko ili anijazie.

Wakati nafuata mifuko, njiani nikakutana na mwanamke na kumpa mifuko ili ikajazwe. Siku ya pili nikaenda kwa mkulima nikakuta ameshajaza mifuko nikaanza kuishona.

Nilipomaliza nikarudi nyumbani nikachukue fedha kwa ajili ya kusafirisha mizigo hiyo nikapata gari aina ya Fuso tukaelewana usafirishaji, nikawasiliana na dalali apokee mzigo, gari likaondoka.

Pia pale kwa jirani yangu kulikuwa na msiba. Nikakumbuka sharti la mganga kuwa ukitokea msiba, gharama zote ni mimi nihusike.

Basi nikaenda msibani nikakuta michango inapitishwa. Nikakaa takriban dakika mbili nikidadisi mwenyekiti wa kamati ya mazishi ni nani. Nikaamua kuuliza wakanionyesha. Tukasalimiana huku akisema maisha ni magumu. Baada ya kukaa pale nusu saa hivi, nikamwambia naomba mwenyekiti unisindikize. Njiani nikaingiza mkono mfukoni nikatoa fedha nikampa kwa matumizi yake.

Kesho yake nikamtafuta ili kujua mahitaji shughuli nzima ya msiba na majukumu yote. Akaniambia msiba unatakiwa kwenda Tabora na gharama yote ni Sh. 800,000. Lakini hadi muda huu nina Sh.150,000 tu na watu wanatakiwa wale chakula, tukishindwa itabidi tuzike hapa.

Nikauliza kama magari yapo Mwenyekiti akasema yanapatikana. Nikamwambia twende tukachague gari zuri mimi nitalipa. Yule mzee alikuwa amekaa kwenye kiti alivyosikia ahadi yangu alinyanyuka nakunikumbatia, na kunichagua niwe msaidizi wake kwenye kamati.

Tukaondoka kwenda kuchagua gari, mzee akachagua Costa moja. Tulipolipata na kukubaliana tukarudi msibani. Kisha nikaenda dukani kwa Mpemba mmoja nikataka mchele na maharage pamoja na mafuta, na vyote vikapelekwa msibani.

Gharama ilikuwa Sh. 500,000 pamoja na kusafirisha Sh.800,000 jumla ikawa Sh. milioni 1.3. Siku iliyofuata watu wakajiandaa kusafiri kwenda Tabora kwa maziko.

**Mpenzi msomaji, hayo ndiyo yaliyomkuta kijana Selestine. Bado kwenye zile ndoo alikuta vitu vingine vya kutisha badala ya fedha. Ni vitu gani hivyo? Fuatilia sehemu ya tano na ya mwisho ya kisa hiki wiki ijayo. Una maoni, Kisa? Ujumbe 0715268581.**

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Uamuzi kuzuia madereva mtandao kufanya kazi ni kuumiza nchi yetu

Nimepata bahati ya kutembea duniani na kila nilikokwenda baada ya kutua, nilitumia usafiri wa mtandaoni, teksi au gari la hoteli ninayofikia.

Katika viwanja vya ndege vya zaidi ya nchi 20 nilizotembelea zikiwamo nyingi za Afrika, sijaona madereva mtandaoni wakikatazwa kuingia uwanjani kubeba abiria.

Nilikwenda mbali zaidi nikauliza kama madereva hao wanakatazwa pia kuingia kwenye kituo kikuu cha mabasi kwa ajili ya kupakia abiria.

Kwenye baadhi ya nchi kama Afrika Kusini katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa OR Tambo, jijini Johannesburg, wanakutangazia kabisa aina zote za usafiri ukiwamo teksi mtandao za kampuni fulani na fulani zinapatikana eneo fulani, hivyo ni wajibu wako kuchagua aina ya usafiri unapowasili.

Kwa nchini kwetu, ni tofauti kabisa. Madereva wa magari ya mtandaoni wanapoingia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) au Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli, wanatozwa faini na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) au uongozi wa stendi.

Kama haitoshi, kuna tangazo limebandikwa kuwa hawaruhusiwi kuegesha gari kwenye viwanja hivyo, lakini wanapoingia na kutoka wanaingiza mapato kwa uwanja kwa kuwa kila gari inalipa Sh. 2,000 kwa saa katika uwanja huo.

Teksi mtandaoni zimetoa ajira kwa vijana wengi na zinalipa mapato mengi kwa serikali lakini kila siku vikwazo vinaongezeka ili kuwalinda madereva teksi ambao hawako mtandaoni.

Sielewi ni kwa nini maofisa wa serikali wa eneo hilo wanazuia teksi mtandao wakati ndizo zingeingiza mapato mengi sana kwa kuwa abiria wanaziita. Pia madereva wa teksi za kawaida wangejiunga huko ingeongeza mzunguko.

Kutokana na hali hiyo, abiria unalazimishwa kuchukua teksi unazozikuta nje ambazo bei zake ni kubwa sana na imefikia mahali wanapokushawishi uwakodishe wanakwambia nitakutoza bei ya Uber au Bolt (teksi za kampuni za mtandaoni) maana yake wanajua kila mtu anafuata urahisi.

Kwa viwanja vya ndege hususan Dar es Salaam hata kama wewe ni mmiliki wa gari la teksi mtandaoni huwezi kumwita dereva akubebe kwa sababu atakamatwa na kutozwa faini ili asiingie humo ndani na wameweka tangazo kubwa la kukataza teksi mtandao.

Kwangu hesabu hizi ni manyanyaso kwa abiria na madereva ambao wengi ni vijana wanajitafutia riziki. Wanalipa kodi ya mapato, wananunua mafuta, wanalipa tozo za Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), jiji na manispaa. Zote hizo ni kodi ambazo lazima zilipwe ndipo gari liingie barabarani.

Badala ya kusaidia biashara hii kustawi, sasa inakufa sijui ni kwa maslahi ya nani? Kwa sasa kampuni maarufu za Uber na Bolt zimeondoa biashara kutokana na kushindwa kuelewana na serikali na wanaoumia ni vijana wengi ambao walitegemea biashara hiyo kuendesha maisha yao.

Tatizo la ajira ni kubwa sana nchini kwa sasa. Hali ya maisha inazidi kuwa ngumu. Watu wanapojikwamua kwa shughuli halali bado wanawekewa vikwazo na hao hao ambao wanatoa vibali kazi hiyo kufanyika.

Kama nchi zenye uchumi mkubwa zinaruhusu teksi hizi kufanya kazi kokote kwa nini kwetu zinazuiwa? Kwa nini itumike nguvu kubwa kuwalinda madereva teksi wa kawaida kwa kuwa wanachama chao bila kuangalia soko huria lilipo?

Hivi karibuni uliibuka mgogoro mkubwa baada ya serikali kupiga marufuku magari kupakia na kushusha kwenye vituo binafsi. Walitakiwa kushusha abiria wote kituo cha Magufuli tu sababu kubwa ni biashara ya teksi na bajaji kuendelea kuwapo kwa sababu wamelipa mapato.

Pia kwenye kituo hicho, teksi mtandao haziruhusiwi kupakia wala kushusha. Kuna watu maalum wa kuwakamata na hii siyo sawa kabisa bali ni kulinda kundi la wachache kwa faida ya wachache huku wengi wakiumia.

Kila siku nchi inazungumzia tatizo la ajira. Teksi mtandao inaajiri vijana wengi na kurahisisha usafiri kwa umma lakini unawekewa vikwazo vingi. Ni ngumu sana kupunguza ukali wa maisha kwa mtindo huu.

Tumeshaingia kwenye biashara huria, hivyo lazima baadhi ya viongozi waondoe urasimu na ubinafsi. Kama hawa madereva wa kawaida wanaonekana muhimu sana, washawishiwe kujiunga kwenye teksi mtandao kuliko manyanyaso tunayoyaona sasa.

Kwa nini wasafiri wa anga wateseke wasipewe uhuru wa kuchagua aina ya usafiri wa kutumia? Kwa nini madereva mtandao wanaolipa kodi kama wengine wanyanyasike nchini mwao?

Mathalani, hivi karibuni nilishuhudia mgogoro wa madereva na askari JNIA iliwakamata wanne na kuwasomea sheria za uwanjani humo kwamba hawaruhusiwi kabisa kupakia abiria.

Yote haya ya nini? Kwa nchi ambayo inatambua biashara ya ushindani na umuhimu wa watu wake kulipa kodi, kunapoongezeka vikwazo kila kukicha ni kuwafanya watu watafute mbinu chafu za kujipatia kipato.

Tuna vijana wengi kwenye eneo hili. Vikwazo vinapokuwa vingi maana yake wataingia kwenye shughuli nyingine mbaya ili kujipatia kipato, hivyo ni muhimu viongozi wanaofanya uamuzi wasiyaangalie maisha kwa jicho lao kwa sababu wana kipato bali kwa jicho la mwananchi wa kawaida kabisa,kwa kuwa wanaishi kwa kodi za watu hao hao.

Haifai kupunguza walipakodi bali kuboresha mazingira ya kuongeza mawanda ya kodi, mazingira bora ya watu kupata fedha na kulipa kodi.

**Mungu ibariki Tanzania**

# HARUSI














Kutokana na mabadiliko katika maisha, mavazi ya harusi si lazima yawe meupe kama ilivyozoeleka. Rangi zozote zinaweza kuleta mvuto na watu wakafurahia kama ilivyo katika picha hizi. PICHA:MTANDAO

# MITINDO

Na Christina Mwakangale



# KWA MPANGILIO HUU UTABAMBA

UNAPOULIZWA kuhusu mavazi, ni muhimu kutambua ni jinsi gani utakavyoyatumia kwa usahihi ili kukupa mwonekano murua.

Ni muhimu kufahamu upangiliaji wa nguo, wakati unapofikiria unataka kwenda wapi, kufanya nini na unakutana na nani?

Ukishajua hilo, basi unaweza kupangilia vyema nguo utakazovaa ili kuongeza mvuto wa taswira yako.

**SHATI JEUPE**

Shati jeupe linaendana na kila rangi ya nguo. Pale kila kitu kinaposhindikana nyanyua rangi nyeupe, Hasa rangi ya nguo ambazo huwa unashindwa jinsi ya kuzipangilia na nguo nyingine.

Unaweza kuivaa na tai ya rangi ya mistari mistari kama unataka kuvaa tai, au unaweza kuvaa pamoja na sweta lenye kola ya V.

**NGUO ZA UGORO**

Rangi ya Ugoro inaendana na rangi yeyote ile angavu. Ni rangi nzuri ya kupunguza ukali wa rangi nyingine, kwa hiyo kama unataka kufanya majaribio ya kuvaa rangi yeyote jaribu kuichanganya na rangi ya ugoro na utaona jinsi utakavyotokelezea.

**NGUO ZINAZONG'AA**

Vaa nguo zenye mng'ao zinazoendana ili uweze kutokelezea vyema. Hakikisha thamani ya rangi ziwe zinaendana, nikiongelea thamani ya rangi namaanisha mng'ao wa nguo uwe unaendana.

Kama umevaa suruali rangi hafifu ambayo haing'ai basi na shati lazima vile vile liwe rangi hafifu.

**RANGI ZINAZOSHABIHIANA**

Vaa kwa kuendana na rangi zinazoshabihiana ili kukupa mwonekano maridadi.

Rangi zinazoshabihiana ni zie zinapingana kwenye duara la rangi, kwa mfano nyekundu na kijani, njano na zambarau, bluu na rangi ya machungwa.



UREMBO

**Na Mary Geofrey**



# Bangili za vifuu zinavyonogesha urembo

BANGILI ni urembo kama ilivyo saa huvaliwa mikononi, wanawake kwa wanaume anayezivaa hupendeza. Zipo za bati, plastiki, shaba, mbao na vifuu pia.

Hata hivyo, wanawake tofauti na wanaume wanapendelea zaidi kutinga bangili mikononi kama njia ya kujipamba.

Kama nilivyosema zinatengenezwa kwa kutumia ngozi, kitambaa kigumu, plastiki, bati, dhahabu, fedha na shaba pia.

Fasheni za bangili hutegemea matakwa ya mvaaji kwa sababu kuna wale ambao wanapenda kuvaa bangili zilizotengenezwa kwa vito vya thamani na wengine wakivutiwa na zilizotengenezwa na vifaa vya asili.

Bangili licha ya kuwa ni urembo wa mkononi, wakati mwingine hutumika kama alama muhimu ya kuwatambulisha watu wa jamii za wafugaji.

Nchini wapo wasanii wa uchongaji ambao hutengeneza bangili kwa kutumia magome ya miti na wakati mwingine vifuu vya nazi.

Bangili za vifuu vya nazi zinapendeza kuvaliwa kutokana na muonekano wake wa kuvutia.

Pia bangili hizo huuzwa kwa gharama nafuu ambayo wengi wanamudu kununua.

Uvaaji wa bangili pia unatakiwa kuzingatia rangi ya nguo, kama mtu ni mweusi anashauriwa kuvaa bangili zenye mng'ao ili kuweza kuwa na muonekano mujarabu.

Ni vizuri kama tutazingatia mpangilio wa rangi katika uvaaji wa bangili na itapendeza kama uvaaji huo utazingatia na rangi ya nguo au viatu.

MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Jinsi ya kukaanga chapati laini

KUJISOSOMOLA kwa chapatti laini iwe kwa chai, supu, maini au maharage ni raha, ila mapishi kwanza. Kuna namna ya kuzikaanga ili zichambuke vyema na kuvutia mlaji.

**MAHITAJI**

Unga wa ngano vikombe vitatu, samli iliyoyeyuka vijiko vya mezani vinne, chumvi kiasi chako na maji ya uvuguvugu.

Matayarisho

Weka unga kwenye bakuli uchanganye na chumvi vizuri, weka samli uchanganye mpaka vibonge au mabuja yote yaishe, weka maji kidogo kidogo ukiendelea kukanda unga mpaka ushikane na ulainike kikamilifu.

Funika unga kisha uweke pembeni kwa takriban dakika 30 au zaidi baada ya hapo ufunue kutoa madonge matatu (ukubwa au kipimo cha madonge kitategemea na mahali au kibao cha kusukumia. Kama ni pakubwa unaweza hata ukafanya donge moja.

Sukuma donge moja moja kama chapati kisha upake mafuta na ukunje kama 'swiss roll' ili kufanya tabaka na gawanya ukubwa unaotaka na ukunje vizuri chapati zako.

Ziache tena kwa takriban nusu saa au zaidi ili zizidi kulainika na bandika kikaango cha kukaangia chapati jikoni hadi kishike moto.

Kikaango kikiendelea kushika moto, sukuma chapati zako unavyotaka (zisiwe nene wala nyembamba sana) na anza kuweka moto na kukaanga.

Chapati ikishika rangi kidogo upande mmoja, igeuze upande wa pili pia ishike rangi na weka samli upande mmoja na uikaange kwa sekunde kadhaa huku ukiikandamiza chini kwa kijiko kikubwa ili ikolee rangi nzuri.

Geuza upande wa pili ufanye vivyo hivyo, kutumia mkono ama kifimbo cha chapati kunja chapati zako mara mbili na uzipige moja baada ya nyingine chapati zipo tayari kuliwa na andaa zikiwa moto kwa maini, maharagwe au chochote upendacho.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Tunza mazingira nyumbani kama ni mfugaji wa mbwa

NYUMBA ni mojawapo ya mambo muhimu sana katika maisha ya binadamu iwe ni ya kupanga au ni ya kumiliki mwenyewe.

Kutokana na umuhimu wa nyumba hiyo na pia ili iendelee kustawi kwa kuwa ni msaada zaidi, inahitaji kujengwa kwa viwango bora ili isiharibike haraka na iwe rafiki wa mazingira.

Inahitaji matunzo ikiwamo kufanyiwa usafi na kukarabatiwa pale inapohitajika kufanyiwa hivyo.

Kama ilivyo katika ujenzi bora kwa nyumba ya binadamu, kadhalika na kwa wanyama, nao baadhi wanahitaji kuishi katika nyumba ili kulinda ustawi wao.

Mtaalam wa kufuga mbwa, Richard Chacha, anasema mbwa wanaofungwa kwa ubora wanatakiwa kufugiwa katika nyumba maalum.

Anasema nyumba ya mbwa mara nyingi zinatakiwa ziwe ndani ya uzio wa nyumba ya mfugaji mwenyewe kwa sababu pia anahitaji uangalizi na kuepusha hatari ya kudhuru watu.

"Ufugaji wa mbwa ni jambo jema kwa sababu lengo lake ni kuimarisha ulinzi katika nyumba, badala ya kutumia au kuajiri walinzi katika suala la usalama. Lakini ukiwa umefuga mbwa inasaidia zaidi na huyu ana faida nyingine kwa sababu akiwa ni mbwa ambaye amefugwa vizuri na kufundishwa, ni rahisi kubaini wahalifu kwa sababu mbali na kupambana nao lakini hutoa kelele za tahadhari," anasema Chacha.

Anasema ili ufurahie kuwa na nyumba bora, lazima pia umjengee makazi bora



ili awe na afya njema.

Chacha anasema baadhi ya vitu muhimu ambavyo unapaswa kuzingatia wakati wa ujenzi wa nyumba ya mbwa ni pamoja na kuhakikisha nyumba yake inakuwa na nafasi ya kutosha ambayo itamuwezesha kujigeuza kwa kadri anavyohitaji.

Anasema nyumba ya mbwa inapaswa kuezekwa kama kawaida japokuwa siyo lazima iwe bati. Pia anasema lazima iwe na mwanga wa kutosha badala ya giza ili kumwezesha kufanya shughuli zake za ndani kwa ndani.

Jambo lingine anasema lazima uhakikishe nyumba inakuwa na sehemu za uwazi wa wastani wa kupitishia hewa.

Mbali na hilo, anasema lazima iwe na mlango na kufuli ambao utakuwezesha kumpitishia wakati wa kumfungulia kwa ajili ya ulinzi na pia wakati anarudi ndani.

Pia anasema lazima kuwe na sehemu nzuri ndani ya nyumba hiyo ya mbwa ambayo itatumika kumtengea chakula ambayo itamwezesha kula kwa uhuru.

Chacha anasema pia lazima uhakikishe kwamba unamwekea kifaa maalum ndani ya nyumba yake ambacho kitatumika kuhifadhia maji yake ya kunywa.

Kwa mujibu wa Chacha, pia nyumba ya mbwa inahitaji kufanyiwa usafi kama ilivyo nyumba ya binadamu, na kuna umuhimu wa kuhakikisha usafi huo unafanywa mara kwa mara ili kumuepusha na maradhi.

Chacha anasema kwa kuwa nyumba ya mbwa hujengwa ndani ya uzio wa nyumba ya kuishi binadamu, ni lazima suala la eneo la kujengewa nyumba hiyo ya mbwa lizingatiwe.


"Tunajua kwamba nyumba za mbwa kwa kawaida huwa siyo kubwa, na wengi wetu hupendelea kujenga au kuezeka na vitu vya ajabu ajabu ambavyo wakati mwingine inaweza kusababisha kuharibu muonekano mzuri na mandhari ya nyumba, pia kama unaona itaharibu ni vema ujenge ambayo unaweza kuihamisha," anasema Chacha na kuongeza:

"Unaweza kuingia katika baadhi ya makazi ya watu, wanakuwa na nyumba nzuri, lakini unakuta hapo katikati ya nyumba wamejengea kibanda cha mbwa kibaya hadi kimeharibu kabisa 'fashion' ya nyumba. Kwa hiyo si vibaya kuchagua eneo zuri la kuweka vibanda hivyo."

Anasema nyumba ya mbwa pia inaweza kupakwa rangi kama zinazotumika kupaka katika nyumba wanazoishi binadamu.


"Kama unathamini kazi kubwa ya ulinzi inayofanywa na mbwa wako nyumbani, lazima pia uthamini maisha yake na makazi yake. Ikiwezekana paka rangi ya nyumba yake, weka hata vyombo na chakula bora kwenye nyumba yake na hii itasaidia awe na afya bora," anasema Chacha.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
HILI NI PAMBANO LA KIRAFIKI NILITEGEMEA TUTAPIGANA HUKU TUNACHEKA LAKINI NAONA UMENUNA KAMA ZIRAILI!
NIKUCHEKEE UNAYETEMBEA NA MCHEPUKO WANGU!
!
BEI YA PETROLI DIZELI
BEI YA VYAKULA
WEWE SEMA KAMA UPO TAYARI KUNIOA NIKUPE BARUA NA HELA UKATOE KWETU.
HAPO HATA NIKIVISHWA SUTI NITAJIHISI KABISA NIMEVALISHWA 'SHELA'
'YULE MTU KAUGUA WAZIMU, ETI ANAKUTAKA NASHANGAA CHIZI KAJULIA WAPI MAPENZI, JIWEKE HAPA UPATE ULINZI POPOTE UENDAKO'
MWAMBIE KWAKE NITAKUWA POYOYO KILA KITU KWANGU 'NDIO'
SASA TUSIFANYE MAMBO YAKAHARIBIKA, NIMEKUDAI KISTAARABU HUKUSIKIA... SASA NIMEKUJA NA HUYU BWANA UNASEMAJE?
ULIYEKUJA NAE MUULIZE KAMA SIMDAI MAHALI ALIYOKWENDA KUOLEA MKEWE
UMENITOA MBIO TUJE KUMFARIJI HUYU 'KAONDOKEWA NA MKEWE NILIDHANI KAFIWA!
MKE KABEBA KILA KILICHO CHAKE UONI KAMA NI MSIBA?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
RAHA YA MPIGA NGOMA, WATU WACHEZE...

HABARI KIMATAIFA

# Majaji Kenya watoa wito 'mtuombee' wanapojitayarisha kutoa hukumu kesho



Majaji wa Mahakama ya Juu nchini Kenya wakiwa kwenye moja ya kikao cha uamuzi kuhusu kesi ya uchaguzi nchini humo, wanatarajiwa kutoa uamuzi wao kesho Jumatatu.

**NAIROBI,** KENYA

KUSIKILIZWA kwa kesi ya kupinga matokeo ya urais kumekamilika Ijumaa huku Naibu Jaji Mkuu Philomena Mwilu akitoa ombi la kuwaombea majaji wanaporejea kufanyia kazi kuandika na kutoa uamuzi wa kesi hiyo.

"Mtuombee tunapoanza awamu inayofuata," alisema Naibu Jaji Mkuu Mwilu na kuongeza kuwa.

"Sio sehemu ngumu sana lakini inahitaji umakini wa hali ya juu na kwa sababu hiyo tunakuomba utuombee Mungu atusaidie tuendelee katika ari ile ile tuliyokuwa nayo katika mwaka mmoja uliopita na tuwe na utambuzi wa hali ya juu sana, tutarudisha kwa Kenya hukumu ambayo si tofauti na kile ambacho Wakenya wanatarajia."

Mwilu katika hotuba yake ya mwisho, alieleza pande zote kwamba katika Mahakama ya Juu, wanafanya kazi kama timu na kwamba hakuna aliye na kura ya turufu.

"Kila siku, mahakama ilikuwa na msimamizi wa kuhakikisha unafuata unachostahili kufanya. Kama hukuona, leo nilikuwa msimamizi. Siku ambayo wengi walicheka, Dkt. Smokin Wanjala alikuwa msimamizi. Tunafanya kazi kama timu hapa, tunafafanua majukumu ili tusiongee kwa wakati mmoja. Hakuna hata mmoja wetu aliye na kura ya turufu lakini tunaye kiongozi wa timu," alisema.

Mwilu alipongeza vyama kwa jinsi walivyoendesha shughuli zao.

"Kama kulikuwa na tabia mbaya, hatukuziona. Tunawakushukuru kwa kufanya kazi ndani ya muda uliowekwa na tuliowapa. Ikiwa uliona au kupata shinikizo kwa sababu ya muda, jilaumu kwa sababu mlitupa siku 14 kufanya kile kinachopaswa kufanywa kwa mwaka mzima, kama ungetuuliza sisi."

Kwa upande wake, Jaji Mkuu Martha Koome, aliiomba nchi iwaombee wanapotoa hukumu ambayo inakuza alichodai kuwa ni "Katiba yetu na inakuza demokrasia yetu na kuleta maelewano nchini."

Kesi hiyo imeendelea kwa muda wa siku tatu huku mawakili wakiwasilisha hoja za kuunga mkono pingamizi zao na upande wa walioshtakiwa nao, wakijitetea.

Wakati wa kesi hiyo siku ya Ijumaa, mawakili wa walalamikaji walishutumu tume ya uchaguzi kwa kukosa kutii maagizo ya kufungua seva ili kuchunguzwa.

Mawakili wanaomwakilisha mwanasiasa mkongwe Raila Odinga waliitaka mahakama kubatilisha ushindi wa Rais mteule William Ruto, kwa madai kuwa kulikuwa na kasoro.

Katika majibu yao, mawakili wa walalamikiwa, ambao ni pamoja na Ruto na tume ya uchaguzi, walijitetea wakiiomba mahakama kutupilia mbali kesi hiyo kwa sababu hakuna ushahidi uliotolewa kuthibitisha uchaguzi huo uliibiwa.

Kinachosalia sasa ni kusubiri uamuzi ambao unaweza kubadilisha hali ya kisiasa ya Kenya.

Sasa jukumu limebakia kwa majaji saba ambao sasa wanafanyia kazi kilichowasilishwa mbele yao kabla ya mahakama hiyo ya Juu Zaidi kutoa umauzi wake.

Hukumu itatolewa kesho Jumatatu.

Iwapo Mahakama ya Juu itaidhinisha uchaguzi wa Ruto, ataapishwa Septemba 13.

Na iwapo uchaguzi huo utabatilishwa, Wakenya watalazimika kurejea kwenye uchaguzi ndani ya siku 60.

**IEBC YADAI TIMU YA RAILA IMETOA USHAHIDI WA UONGO**

Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka nchini Kenya siku ya Ijumaa, ilishutumu timu ya wanasheria ya Muungano wa Azimio kwa kuwasilisha kumbukumbu za uongo 'fake logs' baada ya uchunguzi wa tovuti ya umma.

Wakili Phillip Murgor alikuwa ameonyesha mahakama kile alichodai kuwa ni kumbukumbu kutoka kwa seva ya IEBC ambayo ilionyesha kuwa raia wa kigeni kadhaa walikuwa wametumia mfumo huo siku kadhaa kabla na baada ya uchaguzi.

Hata hivyo, Wakili Dennis Nkarichia wa IEBC alidai kuwa kumbukumbu hizo hazikuwa sehemu ya ripoti ya uchunguzi iliyowasilishwa mahakamani na msajili.

Hii ilisababisha Jaji Isaac Lenaola mwishoni mwa mawasilisho kumtaka Murgor kwenda kwenye ukurasa wa msajili ambao ulionyesha kuwa raia wa kigeni waliingilia uchaguzi kabla ya siku ya uchaguzi na si baada kama timu ya Azimio ilivyodai.

Kisha Murgor akafafanua mahakamani kwamba ripoti aliyowasilisha si ile ya mahakama bali ni kumbukumbu zao wenyewe ambazo alidai pia walizipata kutoka IEBC.

**UPANDE WA IEBC ULISEMA KUWA:**

"Ufikiaji wa seva iliwezeshwa. Mawakala walipewa ufikiaji uliosimamiwa wa seva," ilisema.

Wakili wa IEBC Dennis Nkarichia, pia aliongeza kuwa ukaguzi wa kumbukumbu za ufikiaji seva haukuonyesha shughuli zozote za kutiliwa shaka kulingana na ripoti ya msajili wa Mahakama ya Juu.

Juzi timu yake ya wanasheria iliruhusiwa kuwasilisha ushahidi mpya kuonyesha kwamba matokeo ya mwisho ya uchaguzi ya Tume ya IEBC yalikuwa na dosari.

Katika matangazo ya moja kwa moja wakionyesha kwa majaji wa Mahakama ya Juu, mawakili wa Odinga walidai kuwa kifaa kimoja cha kuwatambua wapigakura kilitumiwa kutuma matokeo kutoka kwa vituo viwili vya kupigia kura vilivyo umbali wa mamia ya kilomita.

Mawakili wake pia waliwaonyesha majaji kile walichosisitiza kuwa, makosa ya hesabu katika baadhi ya vituo vya kupigia kura, wakisema kuwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) ilitumia takwimu bandia kumtangaza William Ruto kuwa rais mteule.

Mawasilisho hayo yalitolewa huku timu ya Odinga ikiteta kwamba ukiukaji wowote wa katiba ni msingi tosha kwa Mahakama ya Juu kubatilisha uchaguzi.

Wakati huohuo, timu ya Muungano wa Azimio imejikuta kwenye utata kwa kudaiwa kutoa ushahidi wa uwongo na Tume ya IEBC.

MAKALA

# WIZI NA UFISADI UNAFUNDISHWA NA SISI WENYEWE



Na Magabilo Masambu

UPIGAJI hatua katika maendeleo ya nchi una uhusiano wa karibu sana na uadilifu wa viongozi serikalini pamoja na wananchi kwa ujumla. Kinyume chake maendeleo ama yanakwenda taratibu au yasipatikane kabisa. Wanaoiba inawezekana wanafanya maendeleo yao binafsi, wakati maendeleo ya taifa yakisinyaa.

Nakubaliana kwamba wizi na ufisadi hauko Afrika pekee bali duniani kote lakini pengine tunazidiana kiwango na kasi ya wizi wa mali za umma. Hata hawa tunaowaona kuwa ni waaminifu na kwamba wamefanya maendeleo mpaka wanapata ziada ya kutusaidia, walituibia wakati tukiwa usingizini. Tulipofungua macho tukakuta wameondoka na mali zetu nyingi sana.

Jambo hili linanifanya niyakumbuke maneno ya Desmond Tutu mwanaharakati na aliyekuwa kiongozi wa kidini Afrika Kusini, aliwahi kusema: "When the Missionaries came to Africa they had the Bible and we had the land. They said Let us pray; we closed our eyes. When we opened them we had the Bible and they had the land."

Hii ina maana kwamba, hata majambazi leo wanaopora ama mali za watu binafsi au za umma wanaonekana wa maana sana wanapotoa misaada kanisani au msikitini na mahali pengine. Rafiki yangu mmoja aliwahi kuniambia Afrika ni sehemu pekee wezi wakubwa hasa wa kisiasa hulindwa lakini mwizi wa kuku anaadhibiwa. Sijathibitisha maneno hayo labda kuna siku nami nitahakikisha.

Sasa Wizi na Ufisadi unafundishwaje? Kwanza, tuna utamaduni kwenye jamii zetu za kiafrika hasa Tanzania ninayoijua, wengine sijui sana wakoje. Tanzania hapa katika mila na desturi zetu ni kwamba katika familia nyingi, ikitokea bajeti imekuwa ndogo pengine kinachopatikana hakitatosheleza wanafamilia wote, basi baba au wakubwa wa familia ndio wanapewa kipaumbele watoto wanafuata.

Tulipokuwa wadogo tulikuwa tunafundishwa kula ugali kwa mchuzi, yaani unawekewa kibakuli kimejaa mchuzi wa nyama au samaki unakula ugali mpaka ukishiba ndiyo unapewa kafinyango kamoja ka nyama ili wakati unakwenda kucheza angalau na wewe uringishie wenzio kwamba kwenu walipika nyama.

Ni kweli kwamba upande mmoja unamfundisha mtoto kubana matumizi, kwamba kula nyama nyingi ni kumfundisha ufisadi na ulafi. Lakini upande mwingine, yule mkubwa anaona ana haki hiyo kwa kuwa yeye ni mkubwa. Tafsiri yake ni kwamba, siku akishika madaraka atakuwa anajilimbikizia huku ikiwa kazi ngumu walioko chini yake kumkemea kwa sababu tumeshazoeshwa wadogo kula kwa mchuzi huku nyama zikiliwa na wazee.

Mtoto naye akikua, atakuwa hali mchuzi tena, bali nyama kubwa kubwa tena zilizonona. Basi utaratibu unakuwa huo mpaka atakapoona kwamba ametosheka ndiyo anatoa salio kwa walioko chini kwa maana ya wananchi wa kawaida. Wakati mwingine nyumbani eti mzee wa familia akikosa pesa ya kutosha kilo ya nyama, ananunua robo halafu anambatanisha na dagaa au maharage kisha maelekezo ni kwamba nyama ni ya baba watoto wale dagaa na maharage.

Tuwafundishe watoto kwa vitendo tangu wangali wadogo kwamba ikiwa baba hana pesa ya kununua kilo moja isiwe tabu nunua robo, nunua hao dagaa na maharage. Wakati wa kula, mnagawana wote na watoto wajue kwamba baba yetu huwa akipata kidogo tunagawana. Kwa jinsi hiyo watoto watajua kwamba kinapopatikana kidogo tunagawana. Akiwa kiongozi atajua kwamba hiki kinachopatikana chafaa kuwa kwa manufaa ya wote.

Kula peke yako kwa sababu huna uwezo wa kumpatia kila mmoja kwenye familia ni kuwafundisha watoto ubinafsi unaozaa wizi na ufisadi. Ukinunua mhindi wa kuchoma hata mmoja barabarani, peleka nyumbani waite watoto wako wote, agiza kisu kata vipande vidogo vidogo kila mmoja apate. Watajifunza kwamba baba amekosa pesa ya kutununulia kila mmoja mhindi wake lakini kila mmoja amepata kidogo. Watafurahi lakini zaidi watajifunza kwamba kikipatikana kidogo ni chetu wote. Baada ya malezi ya nyumbani ni shuleni pamoja na vyuoni. Hapa napo ni sehemu nyingine ya kufundisha na kujifunza ufisadi na wizi bila kujua. Shuleni na vyuoni ni sehemu muhimu sana ya kuwaandaa viongozi wetu wa baadaye. Uzoefu na historia vinaonyesha viongozi wengi wa ngazi ya kitaifa, walianza kuwa viongozi katika taasisi za elimu hasa viongozi wa kisiasa, ukiachana na wale wanaoteuliwa. Kwa hiyo kama nchi ni kuweka mifumo mizuri ya kuwapata viongozi kutokea huko, watakaokuwa si wezi wala mafisadi.

Huku nako kuna kautamaduni kwamba mwanafunzi ambaye ni kiongozi mara nyingi amekuwa akichukuliwa tofauti na wengine. Tuanzie kwenye chakula. Mwanafunzi akishakuwa kiongozi, tayari akilini mwake anaona anatakiwa kutazamwa tofauti. Wakati wa chakula tulikuwa na utaratibu wa kupanga mistari lakini viongozi wanaona hawana wajibu huo.

Jambo la pili ni kuhusu chakula chenyewe. Kiongozi anaona yeye anayo haki ya kupata chakula kingi zaidi kuliko wenzake eti kwa sababu ni kiongozi. Kwa hiyo yuko tayari wengine hata wakikosa yeye ashibe na ikiwezekana akamwage vinavyobakia. Huo ni ulafi na ufisadi. Pale Ifunda Technical tulikuwa na utaratibu kwamba ukigundulika umefanya hivyo, adhabu yake ilikuwa viboko vya kutosha na unaandikishwa maelezo.

Eneo lingine ni kuhusu makazi. Hawa wanafunzi kabla ya kuchaguliwa huwa wanaishi pamoja na wenzao na hakuna shida yoyote, lakini wakishachaguliwa tu wanapewa maeneo rasmi. Hii ni njia njema lakini kinachotokea wakishapewa hayo makazi, wanajiona ni daraja la juu zaidi, si watu wa kawaida tena na ukitaka kuwaona lazima uwe na ruhusa maalum!

Ndiyo maana leo baadhi ya viongozi ukiwa na shida, kuwaona ni kazi ngumu sana. Huwezi kuamini kwamba ndio wale wale vipindi vya uchaguzi mpaka wanakuna nazi na kusaidia kinamama ntilie kupika ubwabwa. Baada ya uchaguzi hawakujui.

Mwanamuziki Lucky Dube amepiga kibao kimoja kinaitwa 'The Way It Is'. Katika kibao hicho anasema: "Now that you got what you wanted, you don't even know my name." Akaongeza: "Be good to the people on your way up the ladder, because you will need them on your way down."

Jamii imebariki wizi na ufisadi. Tunaopiga kelele ni wale tusionufaika na matunda ya ufisadi lakini wale wanaonufaika wametulia, wanakula taratibu, huku wakiwaona vijana wetu mashujaa na kwamba wameanza kwa muda mfupi lakini wamejenga sana makwao, wana akili sana ya maisha. Wale wanaoonekana waaminifu wakichukuliwa kama washamba na wajinga wasiojua kutumia fursa. Hakika kila mmoja atavuna atakachopanda, utafanikiwa lakini hutafanikiwa yote.

**0689157789 magabilomjalifu@gmail.com ARUSHA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Wivu sumu au kinga katika mapenzi?-2



Na Adam Fungamwango

HUU ni mwendelezo wa makala ya wiki iliyopita ikizungumzia wivu kama ni kinga au ni sumu kwenye mapenzi.

Niliandika kuwa wivu ni kumwonea mtu kijicho, kutotaka mwingine apate au kufanikiwa kwa sababu wewe hujafanikiwa kama yeye. Ni kutaka uwe na kile ambacho mwenzako anacho, au hutaki mwenzako apate kitu chochote. Pia wivu ni husuda.

Tulikuwa na nyimbo mbili zinazozungumzia habari hizo, nazo ni 'Wivu' wa Vijana Jazz na 'Wivu' wa DDC Mlimani Park Orchestra. Zimetumwa meseji mbalimbali kutoka kwa wasomaji wakieleza jinsi wanavyofahamu, au mchango wao kuhusu hilo. Mmoja wa wasomaji hao ni Mose kutoka Kahama aliandika meseji isemayo.

"Wivu si kinga bali ni sumu hasa katika maendeleo na hata jamii kwa sababu utakufanya kukosana na kila mtu na hata kiakili utaathirika." aliandika.

Leo tunaziangalia nyimbo zingine mbili zinazongumzia wivu. Tunaanza na bendi ya Kurugenzi Jazz iliyokuwa na maskani yake Arusha.

"Wivu ukizidi nyumbani mapenzi yapungua, wivu usio na maana waleta hasara.

Umepata kitu gani bibi umepata kitu gani, bibi umemkataza kufanya kazi, eti sababu achelewa nyumbani Matatizo mengi sasa yakukuta, mahitaji washindwa kumtekelezea."

Jamaa anamchana mwenzake aliyemkataza mkewe asifanye kazi. Kilichotokea ni kwamba nyumbani kuna matatizo na mahitaji ya muhimu anashindwa kumtekelezea.

"Wivu ukizidi nyumbani hasara, matokeo yake ni kutoamiana. Wivu unaleta ugonjwa wa moyo, sababu ya kuweka mke rohoni. Tuliza moyo kijana waache wake zenu waende kazini mama."

Anazidi kumwambia kuwa wivu ukizidi ni hasara kwa sababu kinachotokea ni kutoamiana. Unaleta ugonjwa wa moyo kwa sababu ya kuweka mke rohoni. Ni kwamba kila anapokuwa nje ya nyumbani unakuwa na wasiwasi na kupiga simu kumuuliza yuko wapi. Kwa hali ya kawaida hakuna binadamu ambaye anaweza kufurahia hilo, iwe mke au mume. Ina maana humuamini, kitu ambacho wengi hawakipendi.

"Kinababa wivu haufai jana, wivu siyo dawa, waruhusuni waende kazini wake zenu, wakafanye kazi. Maisha ya leo ni kufanya kazi, mke na mume kusaidiana." Hapo ndiyo mwisho wa wimbo huo.

Mwishoni kabisa kinababa wanaaswa kuwa wivu haufai, waruhusu wake zao waende kazini. Binadamu hawezi kuchungwa kama ng'ombe, anajichunga mwenyewe. Maisha ya leo ni kufanyakazi, mume na mke kusaidiana.

DDC Mlimani Park ambao wiki iliyopita walikuwa na wimbo uitwao 'Wivu', leo wana wimbo mwingine wenye maudhui kama hayo unaoitwa 'Naomba Tuaminiane.'

"Wasiwasi wako wa nini we mbwana, naona sasa huna imani nami, kila unaporudi kazini wewe unaniuliza maswali mengi, eti nijieleze nilikuwa wapi, wakati wewe mwenyewe uliniacha nyumbani. Na pia hupendi niwatembelee ndugu zangu, hata maelewano yetu sasa ya tabu."

Hapa ni mwanamama anaonekana amechoka kabisa na tabia za mumewe. Mume akirudi kazini anakuwa na maswali mengi ya mtego, ili ajue tu mke leo alikaa nyumbani, au kuna wakati alitoka, na kama alitoka alikwenda wapi? Jamaa wivu umemzidi kiasi kwamba hataki hata mkewe awatembelee ndugu zake. Na kama ndiyo hivyo sijui kama anaweza kumruhusu aende kwenye shughuli za kijamii za mkewe kama vile sherehe mbalimbali au msiba. Huu ni wivu wa kiwango cha lami.

"Tumekwishakuwa watu wazima sasa, nakutafadhalisha, tuaminiane aye." Ni kiitikio cha wimbo huo, mke akimkumbusha mumewe kuwa wameshakuwa watu wazima, kikichobaki waheshiaminiane na kuheshimiana.

"Najiona sasa sina raha mimi, nikitoka unanipeleleza, Najiona sasa sina raha mie, kunisemasema kila siku bwana ee, mapenzi ya kuchungana siyo mema, nakusihi sasa tuaminine. Ukarimu wako nauthamini, penzi letu liheshimu, iwapo hunithamini basi, iliyobaki kila tunapokwenda tuwe sote."

Mama anazidi kumpasha jamaa ambaye kumbe hata akitoka mkewe anampeleleza anakwenda wapi. Inawezekana kabisa jamaa akawa anamfuata nyuma nyuma ili aone anakwenda wapi, au amemkodishia watu wa kumfuatilia.

Kwa bahati mbaya sana yoyote mwenye tabia hii yanaweza kumkuta makubwa, kwani analitafuta kosa kwa nguvu.

Hebu angalia imefikia wakati mke anamwambia mumewe kama akiona vipi basi kila wanakokwenda wawe wameongozana ili kuondoa sintofahamu ya kutomwamini.

Narudia kusema kwa wanaume na wanawake kuwa mtu mzima na akili zake akikukubali na akasema anakupenda ukawa naye, kiuhusiano wa kawaida au ndoa, ujue ameacha mamilioni ya watu na kukuchagua wewe uwe mpenzi wake, hiyo peke yake inabidi ufurahi na kujiamini kuliko kuanza kumfuatilia. Amini anakupenda mwache huru, kwa sababu kiasili binadamu hupenda uhuru kuliko kitu kingine chochote.

Mwamini kuwa anakupenda na muonyeshe uungwana, ukitaka umtendee kama mtoto mdogo yaani kufutilia kila anachokifanya hutafika naye mbali.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

PRINCE Petit kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja tu na walipomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile, badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoena na mtu yeyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane tu alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani Anapofika umri wa miaka 25, baba yake mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

# Mwisho wa Mauaji-17

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

SIMON alimpa kila alichohitaji msichana yule. Atake nini asikipate. Lakini mapenzi ni mapenzi na pesa ni pesa wanangu. Pesa hulainisha tu pale kwenye mapenzi, lakini pesa haiwezi kuzalisha mapenzi. Hilda akili yake ikawa na rafiki ya mpenzi wake, Martin. Alimpenda tangu siku alipomuona kwa mara ya kwanza akiletwa na rafiki yake Simon.

Macho ya mapenzi yanajuana. Watu wakitazamana tu kila mmoja anajua kuna kitu. Martin alihisi kitu kwa Hilda. Mwanamke ndiyo kabisa, jicho aliloangaliwa tu alijua Martin ana lake jambo.


Ni kweli hakutaka kufanya chochote kwa sababu ni mpenzi wa rafiki yake, na kitendo hicho kingeweza kuvunja urafiki na kuzaliwa uadui. Akajitahidi kupotezea. Siku zote macho yakiona moyo unapenda, moyo ukipenda subira hauna, na subira ikitoweka aibu na woga hukimbia.

Martin alishamhusudu Hilda. Hakuwa na subira tena, siku moja akaamua kwenda peke yake hotelini, wakati Simon akiwa amesafiri. Ni siku ambayo Martin aliona Hilda amefurahi kuliko siku zote kuona amekuja peke yake. Martin hakutaka kuongea chochote pale kwa kuogopa macho ya watu kwa sababu wanafahamu kuwa Hilda ni mpenzi wa Simon, akamuachia namba shemeji yake ili wawasiliane baadaye."

Mpaka wakati huo Prince na Hasnat walikuwa kimya, wakimtazama kwa makini Hidaya aliyekuwa mithili ya watoto waliokuwa wakimsikiliza bibi yao akiwapigia hadithi.

"Nyinyi wanangu ni wakubwa, mnajua baada ya hapo nini kiliendelea. Iligeuka, penzi likawa kati ya Martin na Hilda. Liliwakuta watu walioopendana kweli kweli kutoka moyoni na si mmoja kumpenda mwenzake, mwingine kufuata pesa au mali.

Ni wakati huo huo, kabla hata hajafahamu kama amesalitiwa, Simon akapata matatizo, akakamatwa na kushtakiwa kwa makosa ya kununua mali ya magendo kwa ajili ya kuweka kwenye duka lake, akafungwa jela mwaka mmoja. Huku nyuma penzi likakolea kiasi cha kuamua kufunga ndoa." Hidaya akasita na kutoa kikohozi chepesi.




**"Nyinyi wanangu ni wakubwa, mnajua baada ya hapo nini kiliendelea. Iligeuka, penzi likawa kati ya Martin na Hilda. Liliwakuta watu walioopendana kweli kweli kutoka moyoni na si mmoja kumpenda mwenzake, mwingine kufuata pesa au mali.**

"Alipotoka jela?" Hasnat akauliza haraka haraka.

"We nawe mbea wee, basi tu."

"Mh, maana naona hadithi imekolea, imefika penyewe," binti akamjibu mama yake.

"Alitoka baada ya kukaa miezi minane. Alikuta ndoa imefungwa. Huwezi kufanya chochote wakati tayari watu wameshafunga ndoa. Tena kwa mtu ambaye hukuwa umemuoa, kumlipia mahari au kumchumbia. Ilibidi akubali matokeo. Aliwafuata na kuwaambia yeye hana kinyongo kwa sababu wanawake wako wengi na akampongeza rafiki yake akimwambia inawezekana kama asingemchukua yeye, basi angeweza kuchukuliwa na wanaume wengine wakati yupo jela. Hilo liliwatia moyo wanandoa."

Mh, ilitoka rohoni hiyo mama?" Akauliza Prince.

"Naendelea hivyo nisikilizeni. Miaka miwili baada ya ndoa Martin akapata ajali mkoani Morogoro alikokwenda kibiashara. Gari lake lilipinduka na kuanguka kwenye korongo moja kubwa, akapoteza maisha. Bahati nzuri mwili ulipatikana akazikwa kwa heshima. Hilda akabaki mjane masikini.

Baada maombolezo kumalizika na kila mmoja kurejea kwenye hali yake ya kawaida, Simon akamfuata Hilda na kumhitaji tena. Alikataa, kwa sababu ya kulinda ndoa yake, lakini akambembeleza sana, akimkumbusha kuwa yeye ndiye aliyekuwa wa kwanza kuwa mpenzi wake kabla ya marehemu rafiki yake. Tena kwa kumnyang'anya tonge mdomoni. Akamuahidi atampenda na kumtunza kama rafiki yake. Akamuahidi pia kumuoa, kwa sababu bado Simon alikuwa hajaoa ingawa alikuwa na mahawara kibao."

Neno "alikuwa na mahawara kibao", liliwafanya Prince na Hasnat kutazamana na kuchekea kichinichini. Mama hakujua hilo, akaendelea.

"Wakaishi kwa mwaka mmoja pamoja kwanza bila ndoa. Kabla chochote kufanyika, ndipo Hilda alipopata taarifa sahihi na ushahidi juu kuwa mume aliuawa. Haikuwa ajali ya kawaida. Kilichotokea ni kwamba alitekwa mkoani Morogoro, akauawa na watu wasiojulikana, akawekwa kwenye gari yake. Likapelekwa hadi sehemu yenye korongo, maiti ikawekwa kwenye gari yake ikasukumwa na kuanguka chini ya korongo hilo refu ili ionekane kama ni ajali ya kawaida."

Akawaangalia wanaye, akaona wako kwenye hali ya masikitiko kutokana na hicho kilichotokea.

"Basi wanangu, hiyo ikamuuma sana Hilda. Kumbe 'mchawi' wa mumewe ni huyo anayeishi naye. Alijisikia vibaya sana. Alikuwa anampenda sana Martin. Akaona hawezi kuishi na muuaji. Yeye alidhani ni ajali ya kawaida ndiyo maana alikubali. Kama lilikuwa ni wazo lake atengeneze ajali ili ampate yeye amenoa.

Akaamua kumwambia ukweli na kutaka kuondoka. Simon akaonyesha ngozi yake halisi. Akamwambia iwapo akiondoka, au akitoroka, basi kichwa chake ni halali yake, na atamuua kama alivyomuua mumewe.

Simon alijua ameshinda vita, kumbe sivyo. Hilda akaamua kunywa sumu akafa. "

Hidaya aliwaangalia Prince na Hasnat kwa zamu. Akagundua wamezama kwenye lindi la huzuni baada ya kuambiwa kuwa Martin na Hilda ambao wamesimuliwa kisa chao mwishowe wakafariki kwa nyakati tofauti.

"Masikini hawakuacha hata mtoto." Ilikuwa ni sauti ya Hasnat iliyojaa simanzi.

"Waliacha." Akajibu mama yake.

"Wangapi?" Prince naye akauliza.

"Waliacha mtoto mmoja. Kwa bahati nzuri yupo hai hadi leo hii."

"Masikini we, anaishi wapi?" Hasnat akadakia.

"Ndiyo nakuja huko. Unakumbuka mwanangu Prince nilikwambia kuwa wakati nikiwa msichana nilikuwa nikifanya kazi za ndani?"

"Ndiyo mama."

"Basi mimi ndiyo nilikuwa nafanya kazi kwa Hilda na mumewe Martin na yote haya yaliyotokea nimeyashuhudia mwenyewe. Na hata Hilda alipohamia kwa Simon pia alinichukua kwa kumsaidia kumlea mtoto wake kwani alinizoea sana hakutaka kuniacha mwingine. Aliniita mdogo wake na mimi nilimwita dada na hatukupishana sana umri.

Basi niwaambie tu, mtoto mwenyewe niliyemlea nikiwa mdada wa kazi ni wewe Prince."

Mshtuko uliotokea hapo kati ya Prince na Hasnat ulikuwa mkubwa. Pamoja na kuifutilia hadithi yote hiyo, lakini hawakutegemea kama mwisho wake utakuwa huo.

"Ina maana..." Akauliza Prince kwa kigugumizi akiwa amehamanika.

"Ina maana kuwa Martin na Hilda ndiyo wazazi wako halisi. Martin ndiyo baba yako mzazi na Hilda ni mama yako mzazi."

Kabla hajaendelea kuhoji zaidi, Prince alionekana kushindwa kujizuia, akaanza kulia.

Ilikuwa ni kazi ya Hidaya na binti yake kumbembeleza.

"Pole mwanangu, hii ndiyo dunia, ina makubwa. Wa kale walisema dunia ni tambara bovu. Lakini ashukuriwe Mungu amekuongoza kufika kwa mama yako mdogo. Yote ni mipango ya Mungu. Nadhani sasa umepata jibu kwa nini nilikuwa nakuita mwanangu tangu mwanzo kabisa nilipotambua."

**ITAENDELEA JUMAPILI**

# HARMONIZE AITWA KUIMBA INJILI




MCHUNGAJI na mashereshaji maarufu nchini Tanzania, Emmanuel Matebe, maarufu kama MC Pilipili amesema pamoja na nchi hii kuwa na wasanii wengi wazuri, lakini Harmonize ana uwezo mkubwa wa kuimba muziki wa Injili.


Mchungaji huyo ambaye miaka ya nyuma alikuwa mchekeshaji alisema Harmonize anaonekana hutulia sana kwenye kuandika mashairi.

"Kama ningemchagua msanii na kumwambia atoke kwenye bongo fleva aingie kwenye muziki wa Injili, basi ningemchagua Harmonize kwa sababu anaweza. Wengi ni wazuri, lakini jamaa anaonekana anafikiria sana kabla ya kuandika na kwenye uandishi wake mimi namuelewa sana," alisema MC Pilipili.

Alisema kuwa Harmonize ameshawahi kutoa ngoma ya aina hiyo iitwayo 'Mwaka Wangu', hivyo ni rahisi sana kwake kuendelea kutunga na kutoa nyimbo za aina hiyo.

"Alitoa wimbo wake wa 'Mwaka Wangu' na nasikia hivi karibuni alialikwa Arusha na mchungaji mmoja na kuambiwa aimbe wimbo wake huo, hii inaonyesha kuwa jamaa anaweza. Inawezekana ikawa kuna wengine wanaweza, lakini Harmonize tayari ameshatoa ngoma ya aina hiyo." Alisema.

Wimbo huo umemtengenezea heshima msanii huyo kwa baadhi ya wachungaji, wakiona kabisa kuwa anaweza kuwa mwimba nyimbo za Injili mahiri nchini Tanzania, aliutoa miezi saba iliyopita.



# MC Zungu Mshamba

MSANII na mwimbaji wa nyimbo za singeli MC Zungu juzi ameachia ngoma yake mpya aliyoiita 'Mshamba'.

Ngoma hiyo ambayo imeshaanza 'kutrendi' taratibu, msanii huyo ameendeleza ule msemo wa kiswahili uitwao 'ushamba mzigo'.

Kwenye ngoma hiyo, anashangaa jamaa aliyetoka bushi na kuvamia mji kwa pupa, huku wenye mji wenyewe wakimuangalia tu.

Anashangaa jamaa mmoja aliyeuza simu akanunua vocha, akauza nyumba akanunua gari. Halijui jiji lakini anaogopa kuuliza sehemu kwa sababu ataonekana mshamba, wakati hata watoto wa mjini wenyewe kuna maeneo huwa wanauliza. Matokeo yake mitaa imemchakaza, amepotea.

Hivyo ndivyo MC Zungu anavyomsasambua huyo Mshamba anayemuimba kwenye ngoma yake hiyo.

Ni ushahidi mwingine wa msanii huyo kutaka kujitwalia ufalme kwenye aina hiyo ya muziki, kwani amekuwa akitoa ngoma kibao zinazohiti.

Ngoma zake zilizofanya vizuri na kukonga nyoyo za mashabiki wake na wa muziki huo ni 'Nimpende Nani', 'Bye Bye', 'Nafsi', 'Usiku', 'Sina Hela', 'Wanaogopa Kifo', 'Kama Poa', 'Kwa Ajili Yako', 'Sina Kitu' na nyingine nyingi.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

### CITY ILIMKATAA NEYMAR

KLABU ya Paris St-Germain ilimtoa Neymar kwa Manchester City kabla tu ya tarehe ya mwisho ya dirisha la usajili kufungwa - lakini mabingwa hao wa Ligi Kuu England walikataa ofa hiyo ya kumsajili mshambuliaji huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 30. (***Marca***)

### UNITED ILIMTAKA TOMAS

MANCHESTER United ilishindwa katika ombi la siku ya mwisho la kumsajili mshambuliaji wa Hispania, Raul de Tomas mwenye umri wa miaka 27 kutoka Espanyol. ***(Football Insider)***

### GAKPO HAONDOKI PSV

MSHAMBULIAJI wa Uholanzi, Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 23, anatarajiwa kusaini mkataba mpya kabisa katika klabu ya PSV Eindhoven baada ya kuwindwa na Manchester United, Leeds United na Southampton msimu huu. ***(Eindhovens Dagblad)***

### ZAHA ALITAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur ilitaka kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Wilfried Zaha mwenye umri wa miaka 29 kutoka Crystal Palace kabla ya tarehe ya mwisho usajili. ***(Athletic)***

### GNONTO ATUA LEEDS

LEEDS United ilifanikiwa kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Italia, Wilfried Gnonto kwa dau la pauni milioni nne pekee baada ya kukataa kufikia bei ya FC Zurich ya pauni milioni saba kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18. ***(Football Insider)***

### PALMAS YAIGOMEA BARCA

RAIS wa Las Palmas, Miguel Angel Ramirez, amesema alikataa ofa ya euro milioni 25 kwa mshambuliaji wa Hispania, Alberto Moleiro mwenye umri wa miaka 18, ambaye alihusishwa na Barcelona na Manchester City mapema msimu huu. ***(Marca)***

### JONG AIKERA UNITED

MKURUGENZI wa Soka wa Manchester United, John Murtough, amekubali klabu hiyo ingeachana na mazungumzo ya kumsajili kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25 kutoka Barcelona mapema zaidi kuliko walivyofanya. ***(ESPN, via Express)***

### ZIYECH ALITAJWA EPL

BODI ya Manchester United ilipiga kura ya kumtaka winga wa Chelsea kutoka Morocco, Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka 29. ***(Manchester Evening News)***

### MOURA ALIKUWA SOKONI

KLABU za Newcastle na Aston Villa ziliwasiliana na Tottenham siku ya mwisho kuhusu kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Brazil, Lucas Moura mwenye umri wa miaka 30. ***(Fabrizio Romano).***

### GIL: SIFURAHII SPURS

WINGA wa Hispania, Bryan Gil mwenye umri wa miaka 21 amedokeza hana furaha na Tottenham Hotspur baada ya uhamisho wa pili wa mkopo kwenda Valencia kutofanikiwa siku ya mwisho. ***(Sun)***

### SIMEONE AWEKA WAZI

KOCHA wa Atletico Madrid, Diego Simeone, amekiri anafuata maagizo ya klabu kwa kumtumia mshambuliaji wa Ufaransa, Antoine Griezmann, kidogo ili kuepuka kulipa euro milioni 40 katika kipengele cha mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 ambaye anacheza kwa mkopo hapo kutoka Barcelona. ***(Sport)***

------------------------

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BARCA YAKAMILISHA USAJILI WA ALONSO

**BARCELONA,** Hispania

Ni baada ya beki huyo kuomba kuondoka Chelsea na kurejea katika...

MARCOS Alonso amekamilisha uhamisho wake wa bure kutoka Chelsea na kujiunga na klabu aipendayo ya Barcelona.

**Beki huyo wa kushoto ali kuwa ameondolewa katika kikosi cha Thomas Tuchel msimu huu baada ya kuomba kuhamia Camp Nou kabla ya msimu mpya haujaanza.**

Mkataba wake Stamford Bridge ulikatishwa siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili la majira ya joto, na Alonso sasa ni mchezaji wa Barcelona baada ya kusajiliwa na Blaugrana hao juzi Ijumaa.

Pierre-Emerick Aubameyang tayari alikuwa amehamia Chelsea kama sehemu ya kukamilisha dili hilo la Alonso.

Alonso ametia saini mkataba wa mwaka mmoja wenye kipengele cha kumnunua moja kwa moja kwa thamani ya euro milioni 50.

Alijiunga na Chelsea mwishoni mwa dirisha la majira ya joto mwaka 2016 akitokea Fiorentina na kwa haraka akawa kipenzi chini yaKocha, Antonio Conte, akifanya vyema kama beki wa pembeni huku The Blues wakishinda taji la Ligi Kuu England katika msimu wake wa kwanza.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania ameshinda Kombe la FA, Ligi ya Europa, Ligi ya Mabingwa Ulaya, Kombe la UEFA Super na Klabu Bingwa ya Dunia kwa kipindi alichokaa hapo London Magharibi.

Akiwa ni zao la akademi ya Real Madrid, Alonso anarejea nchini kwao akiwa amecheza mara moja tu kwenye LaLiga katika maisha yake yote ya soka.

Huku Jordi Alba akiwa na umri wa miaka 33 sasa, mhitimu wa La Masia, Alejandro Balde amekuwa akicheza nafasi ya beki wa kushoto wa Barcelona hadi sasa msimu huu, huku Alonso anakwenda kuleta upinzani wa kugombea namba kwenye nafasi hiyo.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
ARSENAL
1 | 2.58
X | 3.36
2 | 2.53

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588 0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# BROJA ASAINI MIAKA 6 CHELSEA

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Albania, Armando Broja, amesaini mkataba mpya wa miaka sita katika klabu ya Chelsea.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 alifurahia msimu mzuri wa mkopo katika klabu ya Southampton msimu uliopita na alikuwa akiwaniwa na Everton, Newcastle na West Ham msimu huu wa joto.

Lakini kuhama hakukutimia na sasa amejitolea hatima yake kwa The Blues, akisaini mkataba mpya hadi mwaka 2028.

Akizungumza na chaneli za klabu ya Chelsea, Broja alisema: "Nimepoteza maneno kwa kweli kufikiria tu. Ni klabu ambayo nimekuwa nikitamani kuichezea maisha yangu yote, klabu ninayoishabikia na klabu ninayoipenda, nimekuwa hapa tangu nilipokuwa mvulana mdogo hili ni jambo kubwa sana kwangu.

"Kuvaa jezi ya bluu ukiwa na kikosi cha kwanza ni ndoto iliyotimia. Inashangaza kila dakika unapopata kucheza uwanjani kwa sababu hii ni moja ya klabu kubwa duniani.

Mwenyekiti wa Chelsea, Todd Boehly aliongeza: "Tuna furaha Armando amejitoa kwa Chelsea. Ni mshambuliaji mchanga na anayesisimua na sehemu kubwa ya mipango yetu kusonga mbele."

# Allegri : Juve imekamilika



**TURIN,** Italia

KOCHA wa Juventus, Massimiliano Allegri anafikiri kuondoka kwa, Denis Zakaria, aliyejiunga Chelsea ilikuwa hatua bora zaidi kwa klabu na mchezaji, akisema kikosi chake cha Bianconeri "kimekamilika" hata baada ya nyota kadhaa kuachana na timu hiyo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uswisi alikuwa mmoja wa waliotoka dakika za mwisho pale Turin, pamoja na viungo wenzake Arthur na Nicolo Rovella, ambao walihamia Liverpool na Monza.

Allegri aliongeza mchezaji mmoja zaidi, katika mkataba wa mkopo wa mchezaji wa Paris Saint-Germain, Leandro Paredes, lakini hata hivyo, bado anafurahia muundo wa kikosi chake.

"Ni vigumu kusema kama nimeridhika na soko," alisema Allegri.

"Klabu imefanya kazi vizuri sana kwa hatua zinazoingia na kutoka. Tulishikilia vijana ambao walikuwa lengo la klabu.

"Kwa Zakaria, kulikuwa na uwezekano (wa kuondoka) kwa sababu alihisi kujitenga kidogo. Alikubali nafasi hii kwa shauku. Ninamtakia yeye na Arthur mafanikio mema.

"Tumefanya uchaguzi wetu na wana furaha. Tumekamilisha kikosi kwa njia bora zaidi."

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# TANZANIA YAPATA MWALIKO SOKA LA UFUKWENI COSAFA

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Ufukweni imepata mwaliko wa kushiriki mashindano ya COSAFA yanayotarajiwa kufanyika kuanzia Septemba 14 hadi 20, mwaka huu katika mji wa Durban, Afrika Kusini, imeelezwa.

**Tayari kikosi cha soka cha wanawake cha Taifa (Twiga Stars), kiko Afrika Kusini kikishiriki mashindano ya ukanda huo katika Mji wa Port Elizabeth.**

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana,Kocha Mkuu wa timu hiyo, Boniface Pawasa, alisema watakwenda kushiriki mashindano hayo mara ya pili na wanatarajia mwaka huu watafanya vizuri zaidi.

Pawasa alisema kwa sasa wachezaji wake wana uzoefu na anaamini hawatarudia makosa waliyofanya kwenye michuano ya mwaka jana.

"Mashindano haya yatatusaidia kuunda timu itakayoshiriki mashindano mengine mbalimbali yanayokuja, pia yatatusaidia kutuweka katika nafasi nzuri kwenye ubora, yatatupandisha," alisema Pawasa.

Kocha huyo alisema wachezaji wake wanaendelea vizuri na mazoezi na anawaomba wadau kutoka sehemu mbalimbali kujitokeza kuangalia mazoezi ya timu hiyo ili kuwaongezea hamasa nyota wa timu hiyo.

"Tumejipanga kwenda kupeperusha vyema bendera ya Tanzania, mwaka jana tuliposhiriki kwa mara ya kwanza tulifika fainali, ni imani yangu safari hii tutarudi na kikombe, kikubwa ni kuongeza umakini," Pawasa alisema.

Aliongeza kiafya wachezaji wake wako vizuri na tangu waanze kambi hiyo hakuna majeruhi hata mmoja.

Alieleza wamepata mwaliko huo kutokana na uhusiano mzuri uliopo kati ya Tanzania Afrika Kusini.



Wanamichezo wa Polisi Tanzania wanaoshiriki mashindano ya majeshi ya nchi wanachama wa Kusini mwa Afrika (SARPCCO), wakipita mbele ya Mwenyekiti wa umoja huo, Kamishna wa Polisi wa Namibia, Monaliza Molebugi (hayupo pichani) katika mazoezi kuelekea michuano hiyo iliyoanza Dar es Salaam jana. **PICHA: ROMANA MALLYA**

# *Malindi FC yaeleza kilichowabeba*

**NA HAWA ABDALLAH,** ZANZIBAR

KOCHA Msaidizi wa Malindi FC, Ali Kisaka, amesema siri ya ushindi walioupata katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya Black Sailor iliyochezwa juzi ni matunda ya kufanya maandalizi ya muda mrefu.

Malindi imeanza vyema ligi hiyo kwa ushindi wa mabao 2-1, shukrani kwa Said Salum aliyefunga magoli mawili huku Rashid Mohamed akiifungia goli pekee Black Sailor.

Kisaka alisema timu yake imejipanga kuanza vyema msimu huu kwa kushinda michezo yake yote ya awali na kuwafanya mashabiki waendelee kuwaunga mkono.

"Mechi ilikuwa ngumu, ilikuwa na ushindani wakati wote, ndio maana tulikwenda mapumziko tukiwa mbele kwa bao 1-0 dhidi ya wapinzani wetu, Black Sailor," Kisaka alisema.

Naye Kocha Msaidizi wa Black Sailor, Saleh Machupa, alisema anaenda kujipanga upya kwa ajili ya kusaka ushindi katika mchezo unaofata dhidi ya Mlandege FC utakaochezwa Septemba 12, mwaka huu.

Wakati huo huo, Kocha Mkuu wa Polisi, Ali Mtuli, alisema anatarajia kukutana na ushindani katika mchezo wao wa kwanza wa Ligi Kuu Zanzibar ambao watakutana na Dulla Boys kwenye Uwanja wa Amaan kuanzia saa 1:00 usiku.

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 04/09/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 5544 | Cremonese vs Sassuolo | 2.95 | 3.40 | 2.24 |
| 14:00 | 3909 | Montpellier vs Lille | 3.11 | 3.47 | 2.15 |
| 14:00 | 5904 | Reading vs Stoke City | 2.90 | 3.15 | 2.39 |
| 14:30 | 1619 | Anderlecht vs OH Leuven | 1.36 | 5.01 | 7.02 |
| 14:30 | 5993 | SV Darmstadt vs Arminia Bielefeld | 1.63 | 3.93 | 4.68 |
| 15:00 | 3806 | Lyngby vs Randers | 2.76 | 3.41 | 2.39 |
| 15:00 | 4214 | Osasuna vs Rayo Vallecano | 2.02 | 3.14 | 3.89 |
| 15:00 | 5496 | Kryliya Sovetov vs CSKA Moscow | 2.85 | 3.40 | 2.30 |
| 15:00 | 5525 | Odense vs Viborg FF | 2.51 | 3.51 | 2.56 |
| 15:15 | 2631 | FC Luzern vs Servette Geneva | 2.09 | 3.51 | 3.21 |
| 15:15 | 3546 | FC Vaduz vs FC Schaffhausen | 2.31 | 3.63 | 2.55 |
| 15:30 | 3723 | Emmen vs AZ Alkmaar | 3.64 | 3.59 | 1.90 |
| 16:00 | 1738 | Brighton vs Leicester | 1.84 | 3.49 | 3.99 |
| 16:00 | 2948 | CD Feirense vs Mafra | 2.33 | 3.18 | 2.93 |
| 16:00 | 4083 | Brest vs Strasbourg | 2.81 | 3.36 | 2.37 |
| 16:00 | 4099 | Reims vs Lens | 3.06 | 3.41 | 2.20 |
| 16:00 | 4685 | Clermont Foot vs Toulouse | 2.77 | 3.27 | 2.45 |
| 16:00 | 4797 | Spezia vs Bologna | 2.90 | 3.20 | 2.37 |
| 16:00 | 4886 | AC Ajaccio vs Lorient | 2.41 | 3.16 | 2.91 |
| 16:30 | 4159 | Augsburg vs Hertha BSC | 2.45 | 3.24 | 2.74 |
| 17:00 | 1420 | Hull City vs Sheffield Utd | 3.85 | 3.40 | 1.90 |
| 17:00 | 3190 | Royal Antwerp vs KVC Westerlo | 1.96 | 3.57 | 3.52 |
| 17:15 | 5177 | Athletic Bilbao vs Espanyol | 1.54 | 3.89 | 6.06 |
| 17:30 | 1669 | St. Gallen vs BSC Young Boys | 3.36 | 3.61 | 2.00 |
| 17:30 | 1709 | Casa Pia Atletico vs FC Arouca | 2.07 | 3.17 | 3.62 |
| 17:30 | 1903 | Grasshoppers vs FC Winterthur | 1.93 | 3.57 | 3.62 |
| 17:30 | 3428 | Sporting Farense vs Covilha | 1.60 | 3.75 | 5.20 |
| 17:30 | 5543 | Lokomotiv Moscow vs Akhmat Grozny | 2.26 | 3.29 | 2.99 |
| 18:00 | 4040 | Rubin Kazan vs FC Alania Vladikavkaz | 1.91 | 3.42 | 3.52 |
| 18:05 | 1256 | Troyes vs Rennes | 4.01 | 3.71 | 1.80 |
| 18:30 | 2657 | Elfsborg vs Malmo | 2.69 | 3.43 | 2.29 |
| 18:30 | 2683 | Manchester Utd vs Arsenal | 2.58 | 3.36 | 2.53 |
| 18:30 | 3251 | Monchengladbach vs Mainz | 2.15 | 3.55 | 3.00 |
| 19:00 | 2442 | Midtjylland vs Aalborg | 1.54 | 4.11 | 5.42 |
| 19:00 | 4667 | Verona vs Sampdoria | 2.02 | 3.40 | 3.45 |
| 19:00 | 4774 | AEL Limassol vs EN Paralimni | 1.51 | 4.23 | 5.84 |
| 19:30 | 3635 | Villarreal vs Elche | 1.33 | 4.94 | 8.66 |
| 19:30 | 5312 | Charleroi vs KAA Gent | 3.15 | 3.41 | 2.15 |
| 20:00 | 1249 | Spartak Moscow vs Zenit St Petersburg | 3.35 | 3.65 | 1.97 |
| 20:00 | 5881 | Santa Clara vs Maritimo | 2.06 | 3.16 | 3.66 |
| 21:30 | 3475 | AEK Athens vs PAS Giannina | 1.26 | 5.21 | 11.02 |
| 21:30 | 4606 | Aris Salonica vs PAOK | 2.47 | 3.12 | 2.87 |
| 21:45 | 2758 | Antalyaspor vs Kasimpasa | 1.74 | 3.63 | 4.43 |
| 21:45 | 4564 | Nice vs Monaco | 2.72 | 3.42 | 2.41 |
| 21:45 | 5464 | Ankaragucu vs Besiktas | 3.87 | 3.52 | 1.88 |
| 21:45 | 5803 | Udinese vs Roma | 3.89 | 3.55 | 1.85 |
| 22:00 | 1651 | Valencia vs Getafe | 1.92 | 3.19 | 4.26 |
| 22:00 | 5511 | Corinthians vs Internacional | 2.15 | 3.05 | 3.25 |
| 22:30 | 5149 | Portimonense vs Famalicao | 2.26 | 3.16 | 3.16 |
| 23:30 | 5573 | Alianza Lima vs Universitario | 1.75 | 3.43 | 4.21 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumapili Septemba 4, 2022
Nipashe



Barca yakamilisha usajili wa Alonso HABARI UK 21



Beki wa Timu ya Soka ya Taifa 9Taifa Stars), Kibwana Shomary (kushoto), akiwania mpira dhidi ya nyota wa Uganda katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezani wa Ndani (CHAN), iliyochezwa kwenye Uwanja wa St. Mary's, Katende jijini Kampala, jana. Stars ilifungwa mabao 3-0. **PICHA: TFF**

# Yanga yakamilisha hesabu kwa Azam

## ●●● Nabi atamba yuko tayari, afichua ubora wa wapinzani wao uko katika...

**Na Saada Akida**

ZIKIWA zimesalia siku mbili kabla ya kukutana na matajiri wa Chamazi, Azam FC, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema amemaliza kazi yake kueleekea mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mechi hiyo itakuwa ni ya raundi ya tatu wakati mabingwa hao watetezi wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mechi zake mbili zilizopita, lakini wakicheza ugenini.

Nabi aliliambia gazeti hili baada ya kuwafuatilia kwa karibu wapinzani wao, amebaini anahitaji kuongeza umakini katika safu yake ya ulinzi ili kujihakikishia usalama.

Kocha huyo alisema washambuliaji wa Azam wanaonekana wana kasi na ili kuwadhibiti, inahitaji walinzi wake kuongeza utulivu wakati timu inapokuwa inashambuliwa.

"Nimewasoma kwa dakika 180, nimeona ubora wa Azam FC ulipo, ninaendelea kuwanoa mabeki wangu kwa ajili ya kuongeza umakini, hii inatokana na washambuliaji wa wapinzani wetu ni wepesi, hatutaki kupata madhara," alisema Nabi. Mtunisia huyo alisema anahitaji kuona wachezaji wake wanacheza kwa kiwango cha juu na kuendelea kupata matokeo chanya kama ilivyokuwa katika msimu uliopita.

"Ni ukweli mchezo huu utakuwa mgumu na wenye ushindani kwa pande zote, ila sisi tuko tayari kwa ajili ya kusaka matokeo bora ndani ya dakika 90, nina matumaini hayo, si vinginevyo," Nabi alisema.

Alieleza ameitazama Azam FC katika michezo yake miwili ya kirafiki na kubaini wana safu nzuri ya ushambuliaji hivyo ni lazima mabeki wake wawe imara kuwadhibiti.

"Nimewaangalia Azam FC katika michezo yao miwili, waliyocheza Zanzibar nilipata bahati ya kushuhudia, licha ya baadhi ya wachezaji wao kuwa katika majukumu ya nchi, ina wachezaji wazuri, tunahitaji umakini katika safu yetu ya ushambuliaji, hii itatusaidia," alisema kocha huyo.

Alieleza katika kipindi hiki ambacho Ligi Kuu Bara imesimama, aliendelea kufanyia kazi madhaifu yake hasa kutokana na kukosa muda mrefu wa maandalizi ya pamoja kabla ya kuanza msimu mpya.

Yanga ilianza msimu mpya kwa ushindi wa mabao 2-1 ambapo waliifunga Polisi Tanzania na mchezo uliofuata walikutana na Coastal Union, waliokubali kichapo cha magoli 2-0, mechi zote zilichezwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

# Taifa Stars 'OUT' michuano CHAN

**Na Adam Fungamwango**

NDOTO za Tanzania kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zimezimika baada ya kuchapwa na Uganda mabao 3-0 katika mechi ya marudiano iliyochezwa kwenye Uwanja wa St Mary, Kitende jijini Kampala jana.

Taifa Stars imeondolewa katika michuano hiyo kwa kichapo cha jumla cha mabao 4-0, ikifungwa goli 1-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumapili iliyopita.

Wenyeji walianza biashara asubuhi tu kwa bao la dakika 16 lililofungwa kwa penalti na kiungo, Moses Waiswa kufuatia kiungo mkabaji wa Stars, Jonas Mkude kumkwatua, Rogers Mato, aliyekuwa akiisumbua safu ya ulinzi ya Tanzania.

Bao la pili la Uganda liliwekwa wavuni dakika ya 55 kwa kichwa na Richard Basangwa baada ya mpira wa faulo uliowapita juu mabeki wa Stars kabla ya kumfukia mfungaji huyo huku Mato akifunga goli la tatu na kukamilisha furaha kwa Waganda.

Kipigo hicho kimefuta ndoto za Taifa Stars kwenda CHAN, mara ya mwisho ilishiriki fainali hizo mwaka 2019 na ilikata tiketi ya kucheza fainali hizo ikiwa ugenini Uwanja wa Omdurman, Sudan chini ya Mrundi, Etienne Ndayiragije.

# Simba yaiweka KMC FC mtegoni

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi chake kikipoteza mechi ya kirafiki ya kimataifa ya pili mfululizo, Kocha Mkuu wa Simba, Zoran Maki, amesema anahitaji kushinda mechi zote za mzunguko wa kwanza katika Ligi Kuu na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika watakayoshiriki.

Simba jana asubuhi ilifungwa bao 1-0 na Arta Solar kutoka Djibouti katika mechi ya kirafiki ya kimataifa iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Maki aliliambia gazeti hili vijana wake hawakucheza vibaya sana, lakini aliweka wazi jambo la kwanza lililowaumiza ni jua kali huku akiongeza kukosekana kwa nyota wake walioko katika kikosi cha Taifa Stars kumechangia.

"Dejan amekosa mabao kama mawili au matatu ya wazi, anaweza kutuliza mpira na kufanya kila kitu sawa, lakini kuweka mpira ndani ya wavu bado, ni tatizo la kisaikolojia ambalo nitajaribu kukaa naye na kumweleweza nini cha kufanya na atakaa sawa," alisema Maki.

Simba inajiandaa kuwakabili KMC katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa Jumatano na Septemba 10, mwaka huu watakuwa Malawi kuwakabili wenyeji Nyasa Big Bullets katika mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042